# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

### Kikao cha Nane – Tarehe 16 Septemba, 2016

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA NA WENYE ULEMAVU**:

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake yaliyochapishwa tangu tarehe 29 Aprili, 2016 kama ifuatavyo:-

(i) Toleo Na. 18 la tarehe 29/04/2016,
(ii) Toleo Na. 19 la tarehe 06/05/2016,
(iii) Toleo Na. 20 la tarehe 13/05/2016,
(iv) Toleo Na. 22 la tarehe 27/05/2016,
(v) Toleo Na. 23 la tarehe 03/06/2016,
(vi) Toleo Na. 24 la tarehe 10/06/2016,
(vii) Toleo Na. 25 la tarehe 17/06/2016,
(viii) Toleo Na. 26 la tarehe 24/06/2016,
(ix) Toleo Maalum Na. 1 la tarehe 30/06/2016,
(x) Toleo Na. 27 la terehe 01/07/2016,
(xi) Toleo Na. 28 la tarehe 08/07/2016,
(xii) Toleo Na. 29 la tarehe 15/07/2016,
(xiii) Toleo Na. 30 la tarehe 22/07/2016,

(xiv) Toleo Na. 31 la tarehe 22/07/2016,
(xv) Toleo Na. 32 la tarehe 05/08/2016,
(xvi) Toleo Na. 34 la tarehe 12/08/2016,
(xvii) Toleo Na. 35 la tarehe 19/08/2016.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu. Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:** Maswali.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 96

**Ukosefu wa Nyumba za Walimu Vijijini**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Ukosefu wa nyumba za walimu katika maeneo ya vijijini unasababisha Walimu kuhama maeneo hayo na hivyo kusababisha upungufu mkubwa wa Walimu, pia Halmashauri nyingi hazina uwezo wa kujenga nyumba za Walimu za kutosha kwa kutumia fedha zao za ndani.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga nyumba za Walimu wa shule za msingi vijijini hasa ikizingatia kuwa vijijini hakuna nyumba ambazo Walimu wanaweza kupanga?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi Mbunge wa Jimbo la Bukene kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakabiliwa na tatizo la ukosefu wa nyumba za Walimu kupitia bajeti zilizotengwa katika kila mwaka. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga shilingi bilioni 13.9 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 1,157 kwa shule za msingi na shilingi bilioni 11.1 zimetengwa kujenga nyumba 661 kwa shule za sekondari nchini. Aidha, kupitia mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES II), Serikali imepanga kujenga nyumba za Walimu 183 katika shule za sekondari kwenye Halmashauri mbalimbali zenye uwezo wa kuchukua familia sita kwa kila nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega katika mwaka wa fedha 2016/2017 imetengewa shilingi milioni 486.3 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Walimu kwa shule za msingi na sekondari.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Zedi swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri na hasa wazo la ku-*design* nyumba moja ambayo itaweza ku-*accommodate* Walimu sita kwa maana familia sita. Sasa swali langu ni kwamba je, Serikali haioni sasa kwamba kuna umuhimu wa kusambaza hii ramani ya *design* hii ambayo nyumba moja inaweza ika-*accommodate* Walimu sita kwa Halmashauri zote na maelekezo maalum ili shule ambazo zipo vijiji sana Halmashauri ziweze kutumia ramani hii na kujenga nyumba? Kwa sababu ukiweza kujenga nyumba mbili tu maana yake tayari ume-*accommodate* Walimu 12?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikiri katika Jimbo analozungumza Mheshimiwa Mbunge na mimi nilikuwa kule. Aliponiagiza yeye mwenyewe nitembelee Jimbo lake; nikatembelea miradi ya afya na kuona mambo mengine na changamoto za miundombinu. Naomba niseme ushauri huu tumeshaufanyia kazi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhakikisha ramani hizi zinakwenda kila Halmashauri. Tunachokifanya ni kuhakikisha tunaweka mkazo sasa, bajeti yoyote inayopatikana lazima tuelekeze katika mfumo wa ramani mpya ambayo kwa kiwango kikubwa ina tija sana katika Halmashauri zetu kuhusu suala la kupunguza tatizo la upungufu wa nyumba za Walimu katika Halmashauri zetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanne Mchemba, swali la nyongeza.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wengi wamejitolea kujenga maboma ambayo wamejitolea kujenga zahanati, nyumba za Walimu na mpaka sasa halmashauri hazijaweza kukamilisha. Je, ni lini sasa Halmashauri zitakamilisha miradi ambayo ni viporo ambavyo wananchi wameweza kujenga? (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli maboma ni mengi na kumbukumbu yangu kati ya tarehe 12 na 13 nilikuwa kule Tabora katika Mkoa wako na nishukuru

sana ushirikiano wako japokuwa ulikuwa na changamoto za kuuguliwa. Katika kupita huko huko katika Mkoa wa Tabora lakini na mikoa mingine tatizo la maboma limekuwa ni kubwa ndiyo maana katika maelekezo yetu tumeagiza kwanza lazima tumalize vile viporo vya mwanzo. Kama maboma ya ujenzi wa zahanati, nyumba za Walimu lazima tumalize hilo kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana mtaona katika maelekeo ya bajeti yetu itakayokuja ya mwaka mwingine wa fedha unaokuja, tutahakikisha suala zima la maboma sio suala katika sekta ya elimu peke yake hali kadhalika katika sekta ya afya tumalize hayo halafu ndiyo tuweze kuanza upya. Haiwezekani wananchi wamefanya nguvu kubwa za kutosha halafu nguvu zikapotea bure; Serikali imeliona hilo na ndio maana tuna mpango mkakati mpana sana kuondoa kero hiyo katika Jamhuri yote ya Tanzania.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mary Nagu.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kufanya bidii yote ya kutengeneza madawati kwa ajili ya watoto wa shule na kwa sababu madarasa hayatoshelezi kuna hatari ya madawati hayo kuharibika. Je, wakati haujafika sasa kuwa na mpango mzuri kama ulivyokuwa wa madawati kutengeneza madarasa hasa pale ambapo tunazingatia wananchi wameshajitolea kwa kiasi kikubwa? Je, ni mpango gani ambao Serikali unaweza ukaufanya ili tuwe na madarasa ya kutosha kuweka madawati ambayo tumeyatengeneza wote? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, kwanza naomba tuongeze juhudi kubwa za Watanzania; Mheshimiwa Rais alipotoa maelekezo kwamba tuondoe tatizo la kero wanafunzi kukaa chini na wengine kukaa katika mawe sasa watanzania tushirikiane kwa pamoja kutengeneza madawati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kwamba zoezi hili limefanikiwa kwa kiwango kikubwa sana lakini tulipongeze na Bunge lako hili kuhakikisha kwamba limeweza kutoa mgao wa madawati kwa Majimbo mbalimbali ili kuweza kupunguza ile kero ya madawati katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tatizo la kwanza ukipunguza maana yake tumetoa tatizo la wanaokosa shuleni, watoto elimu bure tumepata changamoto, tumepata madawati. Lakini sasa hivi tuna tatizo la vyumba vya

madarasa hali kadhalika na vyoo, ndiyo maana katika mpango mkakati uliokuwepo hivi sasa katika bajeti hii ya mwaka wa fedha tunaoondoka nao tunaona kwamba kutakuwa na ujenzi wa madarasa katika maeneo mbalimbali na ujenzi wa matundu ya vyoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naomba niwahimize Watanzania wote, japokuwa Serikali itakuwa na mpango mpana sana kuhakikisha kwamba tunaondoa kero ya vyoo na kero ya vyumba vya madarasa hali kadhalika nyumba za Walimu kama nilivyosema awali, lakini niwaombe Watanzania tuendelee kushirikiana kwa pamoja vile vile kama tulivyofanya katika madawati, basi tufanye tena katika nyumba za Walimu na madarasa. Mwisho wa siku tukipata elimu bora, itakuwa ni kwa maslahi mapana ya nchi yetu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa, Mheshimiwa Antony Calist Komu Mbunge wa Moshi Vijijini swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa James Mbatia.

Na. 97

**Mradi wa Kusambaza Maji Vijiji vya Mande na Tella- Moshi**

**MHE. JAMES F. MBATIA (K.n.y. MHE ANTONY C. KOMU)** aliuliza:-

Tarehe 13/8/2012 Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ilitangaza zabuni Tenda Na. LGA/046/2011/2012/RWSSP/1 katika gazeti la Mwananchi. Tenda hiyo ilihusu mradi wa mfumo wa kusambaza maji na ungehusisha Vijiji vya Mande na Tella katika Kata ya Oldmoshi Magharibi. Hadi sasa mradi huo haujaanza pamoja na ufuatiliaji wa karibu wa Diwani na Kamati za Maji za Vijiji vya Tella na Mande hawakufanikiwa kupata majibu juu ya mradi tajwa.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga mradi huo muhimu kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Antony Calist Komu, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ilitangaza zabuni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa mitatu ya maji yaani Korini, Bori na Tella-Mande ambapo

Kampuni ya Jandu *Plumbers Limited* ya Arusha ilipata Zabuni hiyo. Kulingana na upatikanaji wa fedha, kipaumbele kiliwekwa kuanzia utekelezaji wa mradi wa Korini na Bori ambayo imekamilika. Mradi wa Korini umegharimu shilingi bilioni 1.2 na umekamilika mwaka 2014 na mradi wa Bori umekamilika mwezi Juni, 2016 na kuzinduliwa na mbio na Mwenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi wa Tella na Mande umepangwa kuaanza mwaka 2016/2017 baada ya kukamilika kwa miradi mikubwa miwili ya Korini na Bori. Mradi huo umetengewa shilingi milioni 759.4 kwa ajili ya kuimarisha chanzo cha Masokeni pamoja na miundombinu mingine ya kusambaza maji kuwafikia wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa James Mbatia swali la nyongeza.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Chanzo cha maji Masokeni kuimarishwa kwa shilingi milioni 759 na miundombinu ya kuhakikisha Vijiji vya Mande na Tella katika Jimbo la Moshi Vijijini ni fedha kidogo kwa kuwa eneo lenyewe ni kubwa, mahitaji ni makubwa. Serikali inaji-*commit* vipi kuhakikisha kwamba pamoja na fedha hizi watatafuta chanzo kingine cha fedha ili mradi huu ukamilike kama walivyoahidi hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini, Kata nyingine za Kirua Kusini, Mamba Kusini, Mwika Kusini, Kahe Mashariki, Kahe Magharibi pamoja na Makuyuni ambayo ni Mji mdogo wa Himo ambao unapanuka kwa kasi kubwa tatizo la maji ni kubwa sana na Kata ya Mamba Kusini imebidi Diwani aanze kufanya harambee... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia naomba uulize swali tafadhali.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Ndiyo nauliza swali, Serikali inaji-*commit* vipi kwenye maeneo haya mengine niliyoyataja ambayo maji ni muhimu kwa uhai wao ili waweze kupata maisha endelevu kama raia wengine wa Jamhuri ya Muungano? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa kwamba kwanza walitangaza tenda, halafu mradi ule haujaanza. Hata hivyo, tumeshatoa maelekezo kwa Halmashauri zote ile miradi ambayo haikuanza kwa sababu ya ukosefu wa fedha kwamba miradi hii ndio viwe vipaumbele kwa awamu hii tunavyoanza katika utekelezaji wa bajeti ya 2016/2017, hayo ndiyo maelekezo tuliyoyatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwamba fedha ni kidogo, ni kweli shilingi milioni 759 haiwezi kumaliza mradi kwa mara moja, lakini ni fedha ambayo unaweza ukatangaza ukampa *advance* mkandarasi akaanza kujenga. Sasa hivi tunazo fedha za Mfuko wa Maji ambazo tunapeleka kukwamua miradi yote inayoendelea. Kwa hiyo, naomba sana Halmashauri wakaanze kazi fedha hizi zinatosha kupeleka Vijiji vya Tella na Mande. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu yale maeneo mengine ambayo umesema yana matatizo makubwa. Nayo pia tumetoa maelekezo kwamba kila Halmashauri iweke mpango wake katika kutekeleza awamu ya pili ya *program* ya maji kwamba tukimaliza vijiji kadhaa tunaendelea na vijiji vingine ili tufikishe ile azma kwamba Serikali inataka tukifika mwaka 2020 tuwe na 85% wananchi wanaokaa Vijijini wanapata maji na wanaokaa mijini wanapata kwa 95%. Kwa hiyo, tumeshatoa maelekezo usiwe na wasiwasi Mheshimiwa Mbatia tutakwenda kupeleka maji katika maeneo yote kulingana na namna tulivyopanga bajeti. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea, swali la nyongeza.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Matatizo yaliyopo katika Jimbo la Moshi Vijijini yanafanana na matatizo yaliyopo katika Jimbo la Ubungo maeneo ya Kilungule, Kimara Baruti, Korogwe na Golani, Kata ya Kimara pamoja na Makoka, Kajima na Nova Kata ya Makuburi. Je, Serikali ni lini itawapatia maji wananchi wa maeneo hayo? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Ubungo maeneo mengi tunategemea yatapata maji baada ya kukamilisha huu mradi wa Ruvu Juu ambao tayari umeshakamilika. Tatizo lililopo ni kwamba umeme uliopo pale Ruvu Darajani ni mdogo tuna *pump* kubwa sana ya kuleta maji Dar es Salaam; tumeshaanza kuvuta *line* ya umeme kutoka Chalinze kuleta pale. Tutakapomaliza *line* ya umeme maeneo yote ya Ubungo yale yatapata maji kutoka Ruvu Juu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na shaka.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa John Wegesa Heche, Mbunge wa Tarime Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 98

**Utekelezaji wa Ujenzi wa Mpango wa Mji wa Sirari**

**MHE. JOHN W. HECHE** aliuliza:-

Mji wa Sirari unakua kwa kasi kubwa sana kutokana na kuwa na mapato mengi yatokanayo na ushuru wa forodha na bandari kavu. Hata hivyo Mji huo una tatizo la ujenzi holela kutokana na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kukosa fedha za kupanga mji na kulipa fidia stahiki kwa wananchi wanaotakiwa kuhamishwa:-

Je, Serikali itatoa lini fedha za fidia ili kazi ya ujenzi wa Mpango wa Mji huo ifanyike?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Wegesa Heche, Mbunge wa Tarime Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Sirari ni miongoni mwa Miji midogo inayokua kwa kasi nchini Tanzania kutokana na fursa za kibiashara kati ya Tanzania na Kenya pamoja na uwepo wa bandari kavu katika eneo hilo la mpakani. Mji wa Sirari umetangazwa kuwa eneo la mpango yaani *Planning Area* kwa tangazo la Serikali Na. 176 la tarehe 9 Agosti, 1996.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji wa makazi wa Sirari unafanyika kwa njia shirikishi ambapo wananchi wenyewe kwa kushirikiana na wataalam wataamua kuhusu upimaji wa mji huo yaani *informal settlement upgrading.* Hivyo, hakuna fedha zilizotengwa kulipa fidia kwa sababu hakuna wananchi watakaohamishwa katika zoezi hili ili kuboresha Mji. Wakazi wachache ambao watapisha maeneo ya umma kama barabara na huduma za jamii kwa makubaliano yao watapatiwa viwanja mbadala katika maeneo ya Lemangwe, Ng'ereng'ere na Gwitiri ambako vitapimwa viwanja 2,644.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John Heche, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Mji wa Sirari, Mji wa Nyamwaga na Mji wa Nyamongo, kwanza Mji wa Sirari una wakazi zaidi ya 40,000, Mji wa Nyamongo una wakazi zaidi ya 32,000, Mji wa Nyamwaga una wakazi zaidi ya 25,000 na hii

ni miji ambayo imekua, ni mikubwa sasa kuna nyumba mpaka za milioni 600 pale, lakini kwa sababu tu haijakuwa *surveyed* wananchi hawawezi kutumia zile nyumba kukopa kama *collateral* ili waweze kuendesha biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Mji wa Sirari ulitamkwa kwamba ni Mamlaka ya Mji, hakuna Mkurugenzi, bado ni vijiji kwa kifupi tu na miji yote hii, sasa ni lini Serikali itaifanya ile miji iwe Mamlaka za Miji ili iweze kupanga hii miji na kuipima ili wananchi watumie nyumba zao kukopa benki waweze kukwamua maisha yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; sisi tunaishi mpakani mwa Kenya na Tanzania, upande wa pili tu pale mtu ana kiwanja *square meters* 2,000 anakwenda benki anakopa pesa anaendesha maisha, upande wa Tanzania mtu ana eka 20, 30, hawezi kukopa kwa sababu vijiji vyote havijapimwa. Ni lini Serikali itapima vijiji vyote vya Jimbo la Tarime wapatiwe hati za kimila ili waweze kutumia kwenye mabenki kuendesha maisha yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la kwanza kwamba ni lini sasa tutafanya mamlaka ya mji. Nakumbuka katika wiki hii nilijibu swali kwamba mchakato ule wa maeneo mbalimbali ambao vikao vya Madiwani na vikao vingine vya kisheria vimekaa na kufika katika *RCC* na kuja katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tulituma timu ya uhakiki katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, imani yangu, kwa sababu Mji wa Sirari kama mapendekezo yake yalishafika maana yake ni sehemu mojawapo tunayokwenda kufanyia uhakiki. Kwa hiyo, nithibitishe kwamba ni mchakato unakwenda kwa sababu sija-*specify* katika eneo lako, lakini tumefanya zoezi hili kwa Tanzania nzima, lengo letu ni nini? Yale maeneo ambayo yanatakiwa kupandishwa hadhi sasa yatapandishwa hadhi kwa kufikia vile vigezo vyao vilivyofikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala zima la upimaji. Ni kweli unaposema kwamba huku Sirari ni changamoto lakini upande wa pili imepimwa vizuri, ndiyo maana katika hili tumetoa maelekezo mbalimbali katika halmashauri zetu, waweke mipango mikakati mipana ya kuhakikisha kwamba wanapima maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, hatukuishia hapo, tulichokifanya sasa hivi ni kuhakikisha kwamba tunatafuta *funds* kutoka maeneo mbalimbali, kupitia *DFID* sasa hivi katika maeneo yote ya mipakani, lengo letu ni kuweza kuyaboresha yawe mazingira rafiki yakiwemo maeneo ya Sirari.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili litakapokamilika kupitia mradi huu mpana tutayaboresha na kuyapandisha hadhi maeneo yetu, maana yake ni nini, hata thamani ya ardhi katika maeneo yetu itakua na wananchi wetu wataweza kuhakikisha mazingira yao yanakuwa mazingira rafiki hata zile hati zitapatikana, maana yake hata *investment* ya huku Tanzania itafanana kuwa na *investment* shindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa ndugu yangu Mheshimiwa Heche, naomba niseme kwamba tunaomba ushirikiano wa kutosha, pindi zoezi hili litakapokuja basi niombe halmashauri zote tutoe ushirikiano wa kutosha lengo kubwa ni kwamba tuki-*invest* pesa hizi pesa ziweze kuleta matunda mazuri. Kwa hiyo tufanye subira tu katika mchakato huu unaokuja kupitia *DFID.*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na nimpongeze Naibu Waziri kwa maelezo ya swali la msingi. Tatizo la ujenzi holela wa miji katika Tanzania yetu inakumbwa na changamoto mbalimbali ikiwemo fedha, watumishi kwa maana ya Maafisa Mipango miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu takribani miaka sita tulikuwa tunatafuta fedha kwa ajili ya kuandaa mpango kabambe wa *Master Plan* ya Mji wa Mbulu na hatimaye kushindikana, hivyo ni kwa nini Serikali isifanye mapitio upya kuona rasilimali watumishi kwa maana ya wataalam wa Mipango Miji, fedha za kuhakikisha kwamba miji midogo na miji mikubwa inayopanuka inafanyiwa utaratibu wa mipango miji ili nchi yetu isikumbwe mara nyingi na bomoabomoa zinazojirudia mara nyingi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na ndiyo maana hapa mwanzo nimezungumzia hii programu kubwa ambayo kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunaanza nayo hivi sasa na hii maana yake haitogusa maeneo yale ya pembezoni, isipokuwa yale maeneo ya mipakani kwanza ndiyo yatakuwa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafanya hivi kwa nini, ni kwamba ukipita nchi mbalimbali, maeneo yaliyopangwa yatafurahisha hata unaposhuka katika ndege unapoona jinsi gani mji umepangwa vizuri na bahati mbaya sana katika maeneo yetu mbalimbali miji yetu imekuwa ikijengwa katika *squatter* na ndiyo maana tumetoa maelekezo hasa kwa Maafisa Mipango Miji wa maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa haipendezi, kwa mfano, eneo kama la Kibaigwa ndiyo kwanza linakua na Afisa Mipango Miji yupo pale, anaacha tu ujenzi unaendelea, ndiyo sababu tumetoa maelekezo kwamba kila Afisa Mipango Miji ahakikishe kwamba kupimwa kazi yake na Wakurugenzi tumewaagiza hili, katika zile *performance appraisal* za Maafisa Mipango Miji wahakikishe jinsi gani wametumia taaluma zao kuhakikisha miji yetu inayokua inapangwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali imejipanga tutatafuta *funds,* lakini vilevile tutatumia *human resources* tulizonazo kuhakikisha kwamba watu wetu wanawajibika. Hata hivyo, tunakiri kwamba Maafisa Mipango Miji bado wapo wachache tutajitahidi kutafuta uwezekano wa kadri iwezekanavyo kuongeza nguvu kazi hii ilimradi maeneo yetu yaweze kuwa maeneo rafiki kama nchi ya Tanzania ambayo inakwenda katika Awamu ya Tano ambayo inakwenda kwa kasi zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Tunaendelea, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, sasa aulize swali lake.

Na. 99

**Ujenzi wa Barabara ya Kutoka Igoma – Kanindo**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu aliahidi ujenzi wa barabara ya lami kutoka Igoma – Kishiri – Kanindo kupitia Kata za Lwanhima na Bulongwa.

Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Igoma – Kishiri – Kanindo ina urefu wa kilometa 15 ikiwa ni mzunguko kupitia Kata za Igoma, Lwanhima na Buhongwa katika Jiji la Mwanza. Ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais, Serikali imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali katika bajeti ijayo ya mwaka 2017/2018 ikiwa ni hatua muhimu katika kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hiyo itawezesha Serikali kujua gharama za mradi na kutenga bajeti kwa ajili ya kuanza ujenzi. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa ahadi hii ya Mheshimiwa Rais itatekelezwa kama ilivyoahidiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza, lakini pamoja na maswali mawili ya nyongeza, nikiri kwamba sijaridhishwa kabisa na majibu ya Mheshimiwa Waziri na wala sikubaliani nayo kwa sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu, Nyamagana ndiyo kitovu cha Mkoa wa Mwanza na ni mji unaokua kwa kasi sana, barabara hii haijasemwa leo, imesemwa sana, sasa tukisema mwaka 2017/2018 ndiyo tuanze upembuzi yakinifu tunakuwa hatuwatendei haki wananchi wa Jimbo la Nyamagana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimwombe Naibu Waziri na akumbuke kwamba iko sasa hivi mikakati ya kuboresha miji ukiwemo Mji wa Mwanza, barabara hii itakuwa muhimu sana kwa mkakati wa Serikali wa ukusanyaji mapato, ni lini watakuwa tayari kutumia fedha za dharura kuhakikisha hii shughuli ya kufanya upembuzi yakinifu inafanyika kwa mwaka huu na mwaka ujao barabara hii ianze kujengwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwa sababu zilezile kwamba Mji wa Mwanza ni mji unaokua kwa kasi na mara nyingi tumekuwa tukitumia fedha nyingi wakati wa dharura, tunaposubiri mvua nyingi zinanyesha na kuharibu barabara. Je, ni lini sasa fedha hizi za dharura zitatumika kuimarisha barabara ikiwemo barabara ya kutoka Mkuyuni kwenda Nyangurugulu kutokea Mahina, Buzuruga, lakini ya kutoka Mkolani kwenda *Saint Augustine University* kupitia Luchelele na *Nyegezi Fisheries*?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimjulishe Mheshimiwa afanye rejea katika maeneo ambayo tunafanya mikakati kama Serikali kuboresha barabara zetu likiwepo na Jiji la Mwanza. Kupitia mpango wetu wa *strategic cities* Mwanza ni eneo ambalo tunajenga miundombinu hiyo ikiwa sambamba na Shinyanga, Arusha, Iringa, Mbeya na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, najua kwamba barabara hii ni kweli haijakamilika, lakini nimesema kila jambo lina mpango na Mheshimiwa Mabula, anafahamu Mheshimiwa Rais alivyokwenda pale alisema siyo hizo barabara za eneo la Mwanza isipokuwa hata kujenga daraja katika Ziwa Victoria, nalo linafanyika katika Jiji la Mwanza, mpango mkakati huo unapoenda maana yake kutakuwa na uboreshaji wa hizo barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba najua, amesema ni muda mrefu, lakini anakumbuka huko nyuma alikotoka wapi na hivi sasa yeye yuko wapi. Naamini uwepo wake sasa utasukuma mambo haya yaende vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba Serikali imejipanga ile *ring road* itatengenezwa. Kwa mujibu wa Serikali ilivyojipanga *ring road* tutatengeneza na isitoshe na yeye anafahamu kule *site* kuna watu sasa hivi wanaboresha barabara za Jiji la Mwanza, naomba niwahakikishie watu wa Mwanza, Mheshimiwa Rais alivyotoa kwamba kujenga barabara mpaka kupeleka *airport* baada ya kuvunja sherehe maana yake hiyo ni *commitment* ya Serikali ili baadaye Watanzania wote wanufaike, amesema kwamba tuelekeze eneo hili kwa sababu ni eneo la mkakati, ni azma ya Serikali kuboresha miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naomba nimwambie kwamba katika kipindi cha sasa Serikali ilivyojipanga tutaboresha barabara za aina mbalimbali na katika hilo la kwamba kwa kutumia fedha za dharura tutafanya nini. Juzijuzi nilikuwa katika Jimbo la Mheshimiwa Mabula kule Ilemela, kuna baadhi ya barabara tumefanyia ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia afuate rejea yangu ya kipindi kilichopita, kwamba tutafanya kila liwezekanalo barabara zilizoharibika kwa kadri rasilimali fedha itakavyopatikana tutaendelea kuiboresha. Kwa hiyo, nimwambie mtani wangu, asihofu, awaambie watu wa Mwanza kwamba wamempata jembe lakini Serikali itamsaidia kuboresha Jiji la Mwanza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oscar Mukasa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ipo ahadi pia ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli katika Mji wa Biharamulo ya kuweka kilometa nne za lami wakati akituomba kura. Kwa kuwa sisi habari ya kilometa nne haina mambo makubwa yanayojumuisha mpaka habari ya vivuko kwenye Ziwa Victoria, Naibu Waziri anatuambia nini kuhusu utekelezaji wa haraka na wa siku za karibuni wa ujenzi huo wa ahadi ya Rais?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mukasa hilo swali halijawahi kuulizwa hapa kweli? Au unataka majibu mara ya pili? Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niwape pole watu wa Kagera kwa msiba mkubwa uliotupata na najua sio hilo tu, maana yake maeneo mbalimbali kule yatakuwa yameathirika hasa miundombinu ya barabara. Naomba nimhakikishie, kwa sababu ahadi hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na ndiyo maana Mheshimiwa Rais amejielekeza katika ukusanyaji wa mapato ili mradi kuhakikisha ahadi zake zimetekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, imani yangu, kama mwenyewe anavyosema na kama Serikali yake inavyoonesha jinsi gani ukusanyaji wa mapato ulivyo, tutahakikisha barabara hii inatengenezwa, lakini sitaki kukwambia *commitment* ya tarehe, kwamba lini tutafanya hivyo, lakini katika kipindi hiki naamini itatengenezeka kwa sababu nguvu kubwa inaelekezwa kuhakikisha ahadi za Rais na utekelezaji wa ilani unatekelezeka katika kipindi hiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa matatizo ya Magu yanafanana sana na matatizo ya Nyamagana, Barabara ya Ngudu – Magu – Ngumarwa, usanifu umeshakwisha kukamilika, sambamba na Barabara ya *Airport* – Igombe – Kayenze – Kongolo – Nyanguge ili kupunguza msongamano wa kuingia Jiji la Mwanza na kwa sababu ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, je, barabara hizi zitaanza kujengwa lini kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana yanayotolewa na Naibu wangu, Mheshimiwa Jafo, napenda kujibu maswali ya nyongeza yaliyoulizwa yanayofanana sana na Waheshimiwa Wabunge juu ya ahadi za Mheshimiwa Rais ya barabara zilizoko chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezihakiki, tunazifahamu lakini pamoja na mipango ya halmashauri, Wizara yangu itakuja na mpango mkakati wa namna ya kuzitekeleza barabara hizo zote kabla ya mwaka 2020. Serikali hii ni Serikali ya vitendo, tuliahidi, ni lazima tutatekeleza na ahadi za Rais ni kipaumbele chetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 100

**Sheria ya Ndoa Kuwa Kandamizi**

**MHE. AMINA N. MAKILAGI** aliuliza:-

Sheria ya Ndoa imekuwa kandamizi kwa wanawake na watoto:-

Je, ni lini sheria hii italetwa Bungeni ili ifanyiwe marekebisho?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ni matokeo ya mjadala mpana na shirikishi kupitia Waraka wa Serikali namba moja wa mwaka 1969. Lengo la mjadala huo lilikuwa kupata muafaka kuhusu maudhui ya sheria hiyo ambayo yaligusa imani, mila na desturi za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya miaka zaidi ya 20 kupita tangu sheria hiyo ya ndoa itungwe, Serikali kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria iliifanyia mapitio ya sheria hiyo na kubaini maeneo kadhaa yenye udhaifu na hivyo kuhitaji kufanyiwa marekebisho. Kutokana na maoni hayo ya Tume, Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria iliandaa mwaka 2008 Waraka wa Baraza la Mawaziri uliokuwa na mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

Kwa kuzingatia chimbuko la sheria hiyo, Baraza liliiagiza Wizara kuandaa Waraka Maalum wa Serikali *(White Paper)* ili kupata mjadala mpana na shirikishi kama ilivyokuwa awali. Mapema mwaka 2010 Wizara ilikamilisha maandalizi ya waraka huo ambao pamoja na kubainisha hoja ambazo wananchi wangetakiwa kuzitolea maoni uliainisha utaratibu wa kukusanya maoni ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Desemba, 2010 kabla waraka huo haujajadiliwa na kuridhiwa na Baraza la Mawaziri mchakato wa mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukaanza na kulilazimu Baraza kusitisha kwa muda mchakato wa marekebisho ya ndoa. Serikali ilikuwa na matarajio kuwa wakati Tume ya Mabadiliko ya Katiba inakusanya maoni ya wananchi kuhusu mabadiliko ya Katiba, wananchi wangetoa maoni kuhusu Sheria ya Ndoa, Mirathi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba kukamilisha kazi yake, ilibainika kwamba wananchi wengi hawakujielekeza kwenye maudhui ya Sheria ya Ndoa, hivyo Wizara ya Katiba na Sheria ikaamua kuendeleza juhudi za awali kwa kukamilisha taratibu za kupata maoni ya wananchi kwa utaratibu wa *White Paper,* zoezi hili litakamilika ndani ya muda si mrefu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Makilagi.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada na Bunge lililopita Wabunge tukatunga sheria kali sana ambayo itawabana wale wote waliokuwa na tabia ya kuwaoa watoto. Ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hivi karibuni Mahakama Kuu ya Tanzania iliiagiza Serikali iifanyie marekebisho Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, kama kweli dhamira ni nzuri kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameeleza, ningependa kujua, ni kwa nini Serikali iliamua kukata rufaa badala ya kutekeleza maamuzi ya Mahakama? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa sheria nyingi sana ambazo zinawakandamiza wanawake na watoto, bado zipo katika nchi yetu ya Tanzania, zikiwepo hata sheria za kimila na nyingine na nyingine. Ningependa kujua sasa, Serikali ina mkakati gani na hasa Wizara ya Katiba na Sheria, kuhakikisha inaleta sheria zote kandamizi zinazowabana wanawake na watoto ili sheria hizi tuweze kuzifanyia marekebisho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Amina Makilagi kwa kupigania haki za akinamama bila kuchoka, matunda ya juhudi zenu, wewe mwenyewe Mheshimiwa pamoja na wanawake wenzako yanaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuhusu kesi iliyokuwepo Mahakamani na kwa nini Mwanasheria Mkuu wa Serikali imebidi akate rufani, nimeeleza katika jibu langu la msingi kwamba Serikali inaona tatizo katika Sheria ya Ndoa, si kwamba haioni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichotupeleka Mahakama ya Rufani ni vitu viwili. Kwanza, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, tayari iko katika mchakato chini

ya Wizara yangu na utaratibu tunaoutumia tulidhani itakuwa vyema kwa mshikamano wa Taifa letu tukaendeleza majadiliano kama tulivyofanya wakati wa kuitunga hii sheria ya mwaka 1971. Sisi tunataka tu kupata busara za Mahakama ya Rufani kuhusu suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, haki ya kukata rufani si tu ya wananchi, lakini vilevile hata Serikali pale ambapo inaona kuna kitu ambacho kinahitaji kupewa msimamo madhubuti zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii anaweza akatokea Jaji mwingine wa Mahakama Kuu akatoa uamuzi tofauti kwa sababu wote wako katika maamuzi. Sasa tunachotafuta na anachotafuta *Attorney General* ni kupata sasa maamuzi kwenye Mahakama yetu ya juu katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, ni kweli kabisa bado kuna baadhi ya sheria zinamkandamiza mwanamke lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Amina Makilagi na wanawake wenzake kwamba tumepiga hatua kubwa mno toka uhuru katika kuhakikisha kwamba mwanamke anapata haki sawa kama ambavyo Katiba yetu inavyosema chini ya Ibara ya 13.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke, tumefanya mabadiliko ya sheria nyingi, tukumbuke Sheria ya Ardhi namba Nne (4) na namba Tano (5) imeondoa kabisa ubaguzi uliokuwepo kwa mwanamke. Sasa hivi mwanamke ana haki sawa chini ya sheria hizo. Leo si kawaida tena kwa mume akatoka tu asubuhi akauza nyumba, akauza kiwanja bila kupata ridhaa ya mama na mama akienda Mahakamani hiyo *sale* ama mauzo hayo hayana maana kabisa. Leo hii akinamama talaka haitokei akaondoka hivi hivi lazima kugawana *matrimonial property,* hizo zote kwa kweli ni faida ambazo tumezipata katika mabadiliko mbalimbali ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii nenda Jela; wafungwa wengi wanaotumikia vifungo virefu katika nchi hii ni wale ambao wana makosa ya kunyanyasa akinamama. Namshukuru Mheshimiwa Makilagi ameelezea kuhusu sheria tuliyobadilisha juzi tu hapa Sheria ya Elimu ambapo leo hii mtoto wa kike aliye sekondari, aliye shule ya msingi, akipata mimba ole wako wewe uliyefanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote hii ni kulinda na baada ya muda si mrefu tutaleta Muswada hapa wa Huduma ya Msaada wa Sheria ambayo nakuhakikishia utakuwa mkombozi mkubwa hasa kwa akinamama walioko vijijini ambao katika mfumo tulionao usiojali mtu kutokujua sheria; kwamba *ignorance of the law is not defence,* akinamama wengi watafaidika sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib Haji.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Katika imani ya dini ya Kiislam, suala la ndoa na mirathi ni jambo ambalo halina mjadala wala mbadala. Je, mabadiliko yote ya sheria yanatuhakikishiaje kwamba hayataingilia uhuru na imani katika dini ya Kiislam? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu kwa kifupi sana Mheshimiwa Mbunge kwamba hii ndiyo sababu. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali anakwenda Mahakama ya Rufani akidai si moja kwa moja, lakini kama nilivyowaeleza hapa kwamba mchakato tuliouanza Serikali wa majadiliano sisi Watanzania, maridhiano utumike badala ya sisi kuja na Muswada, wanaosema ndiyo, ndiyo tukapitisha sheria hapa, nadhani nimeeleweka na Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa sasa aulize swali lake.

Na. 101

**Ahadi ya Kujenga Mahakama ya Wilaya ya Chunya**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Katika bajeti ya 2013/2014, Serikali iliahidi kujenga Mahakama ya Wilaya ya Chunya.

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Mahakama ya Tanzania ni kusogeza huduma za utoaji haki karibu na wananchi kwa kujenga miundombinu na kuhakikisha kwamba haki inapatikana kwa wote na kwa wakati. Katika kusogeza huduma, Serikali imedhamiria kujenga Mahakama Kuu kila Mkoa, Mahakama ya Wilaya kila Wilaya nchini na Mahakama za Mwanzo kila Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika mwaka wa 2014/2015 tuliahidi kujenga Mahakama za Wilaya na za Mwanzo katika sehemu mbalimbali nchini

ikiwemo Wilaya ya Chunya. Hata hivyo ahadi hiyo haikuweza kutekelezwa kikamilifu kutokana na upatikanaji hafifu wa fedha za maendeleo. Mahakama katika mwaka 2014/2015 ilipata asilimia nane tu ya fedha za maendeleo zilizotengwa, hivyo haikuweza kutekeleza miradi yote iliyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Chunya umezingatiwa katika mpango wetu wa ujenzi kwa mwaka 2016/2017.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, swali la nyongeza.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na pia nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini pamoja na majibu hayo nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amenihakikishia kwamba Serikali imetenga fedha sasa kwa ajili ya kujenga Mahakama ya Wilaya katika Wilaya ya Chunya, je, ni lini Mheshimiwa Waziri atakuja Chunya ili nimwonyeshe viwanja vilivyo ambavyo Halmashauri imetenga kwa ajili ya kazi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Jimbo langu lina tarafa mbili, Tarafa ya Kiwanja na Tarafa ya Kipembawe. Tarafa ya Kiwanja ina Mahakama za Mwanzo mbili, moja iko Chunya, nyingine iko Makongorosi. Tarafa ya Kipembawe haina Mahakama ya Mwanzo hata moja. Sasa je, Serikali inasemaje kuhusu kuleta Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Chunya ili Halmashauri iweze kumtengea eneo la kuweka Mahakama hiyo katika Tarafa ya Kipembawe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimefarijika sana kumsikia Mheshimiwa Mbunge akisema viwanja tayari wanavyo na hivi majuzi tu nimetoka kujibu swali la Mbunge wa Temeke nadhani, nikielezea tu kwamba ni vizuri Wabunge sasa hivi mkahamasisha Halmashauri zenu kutuainishia viwanja ambavyo tayari vina hati iweze kuwa rahisi kwa Mahakama kuweza ku-*identify* maeneo hayo na kuweza kujenga maana pesa angalau sasa hivi tunayo ya kuweza kuanza ujenzi wa Mahakama za Mwanzo, Wilaya na hata Mahakama Kuu. Na tunashukuru kwamba kiwanja anacho Mheshimiwa Mwambalaswa, nitamfikishia ujumbe huu Mtendaji Mkuu wa Mahakama. Ningefurahi kama rai yake aliyoitoa hapa itafuatiwa na barua ili itiwe na kumbukumbu kabisa kwenye mafaili yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusu Kipembawe kwamba hakuna Mahakama ya Mwanzo, ningemwomba, hiki ndiyo kipindi ambacho Mahakama inaangalia *priorities* tuanzie wapi katika kujenga jumla ya Mahakama 50 za mwanzo. Tafadhali tunaomba alete andiko la hayo mahitaji yawekwe pia kwenye *file* tuweze kuliangalia pamoja na mambo mengine.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi, nina swali moja la nyongeza. Tatizo la ukosefu wa Mahakama katika Wilaya ya Chunya ni sawasawa na tatizo lililopo katika Mahakama ya Herujuu. Jengo lililokuwepo la tangu enzi za ukoloni limebomoka kabisa hivyo huduma ya Mahakama wanakaa chini ya miti. Je, ni lini Serikali itatoa pesa kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Herujuu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri mbele yenu kwamba hali ya miundombinu ya Mahakama nchini si nzuri. Nikielekeza macho tu, upande wa Mahakama za Mwanzo tunahitaji ili tuwe na *access to justice* sawasawa tuwe na Mahakama za Mwanzo katika kila Kata. Tuna kata zaidi ya 3,900 nchini lakini Mahakama tulizojenga mpaka sasa hazizidi 900, kwa hiyo pengo ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Josephine Genzabuke, kuhusu mahitaji halisi katika eneo lake, tunaomba atuandikie hiki ndiyo kipindi ambacho tunaangalia mahitaji kufuatana na *demand* iliyopo katika maeneo yote tuliyonayo. Kwa hiyo tunasubiri ndani ya siku mbili, tatu atatufikishia hayo mahitaji ya jimbo lake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, Mbunge wa Kojani sasa aulize swali lake.

Na. 102

**Maslahi Yanayoendana na Vyeo vya Askari Polisi**

**MHE. HAMADI SALIM MAALIM** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Askari wa Jeshi la Polisi hucheleweshwa maslahi yanayoendana na vyeo vyao pindi wanapomaliza mafunzo kwa ngazi mbalimbali kama vile Koplo, *Sajent, Staff Sajenti, Meja* na vingine?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamadi Salim Maalim, Mbunge wa Kojani, kama ifuatavyo:-

Kwanza nikiri, ni kweli kumekuwepo na matatizo ya Askari kupanda vyeo na kucheleweshewa malipo yanayoambatana na kupanda vyeo hivyo. Askari Polisi kupanda vyeo kama ilivyo kwa watumishi wengine wa umma na vyeo hivyo kuambatana na kuongezeka kwa maslahi kulingana na cheo walichopandishwa. Kwa mwaka 2014/2015, jumla ya askari 1,657 wa Vyeo vya uongozi mdogo walipandishwa vyeo mbalimbali na mwaka 2015/2016, Askari wapatao 3,017 walikuwa katika Vyuo vya Polisi wakihudhuria mafunzo na hivyo kupandishwa vyeo kuwa maafisa na wakaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwepo na ucheleweshaji kama nilivyosema wa mafao haya yanayolingana na vyeo walivyopanda kijeshi na Serikali mara zote imekuwa ikijitahidi kurekebisha mishahara ya vyeo vipya kwa haraka iwezekanavyo kwa askari waliopanda vyeo. Yapo matatizo ya kiufundi yanayojitokeza wakati wa zoezi la kurekebisha mishahara na kutokea baadhi ya askari kutorekebishiwa mishahara yao na hivyo juhudi hufanyika ili kutatua tatizo hilo mara moja na mhusika anapowasilisha malalamiko yake Polisi ama Makao Makuu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hamad Maalim, swali la nyongeza.

**MHE. HAMADI SALIM MAALIM**: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini pia naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Wizara imekubali kwamba kumekuwa na ucheleweshaji wa mishahara kwa askari hawa wanaopandishwa vyeo, ni kwa nini basi askari hawa wacheleweshwe mishahara yao wakati kila bajeti inapopitishwa tayari nyongeza ya mishahara inakuwa tayari imeshaingizwa katika bajeti ile? swali namba moja.

Pamoja na kwamba Wizara pia imekubali kucheleweshwa kwa mishahara kwa askari hawa, kwa nini basi wanaporekebishiwa mishahara yao washindwe kulipa zile *arreas* za ile miezi ya nyuma au miaka ya nyuma ambayo imepita kabla ya kurekebishiwa mishahara yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mbunge kwa kufuatilia na kuwasemea vizuri vijana wazalendo hawa wanaojitolea kwa ajili ya Taifa letu. Mwenyewe nimezunguka katika mikoa mbalimbali na nimepata fursa ya kuwasikiliza. Matatizo ya aina hiyo si hilo

tu, lakini kama Wizara tunaandaa utaratibu wa kila mkoa kuwa na watu wanaofuatilia masuala ya askari ili askari yeye kazi yake iwe ni kulitumikia Taifa na kuondokana na ucheleweshwaji wa marekebisho haya ambayo kimsingi yanatokana na taarifa kamili zinazokusanywa zinazohusu mabadiliko hayo kuchelewa kupatikana na kufikia Utumishi ambao wanahusika kwa ujumla wake kutambua nani anatakiwa alipwe kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapanga si hilo tu la mishahara pamoja na stahili zingine zingine ambazo wanazipata zikiwemo wanapokwenda kufanya kazi nje ya kituo chake, anapokwenda kwenye *operation* maalum, anapopata haki yake anayo stahili, kuwa na malalamiko mengine hata ya posho anayostahili ambayo inatakiwa kimsingi iendane kwa asilimia ya mshahara wake, mshahara unapopanda posho ile inabaki *constant* licha ya kwamba ilitakiwa iwe kwenye uwiano wa asilimia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Upendo Peneza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Pamoja na Serikali kufanya jitihada za kuwapa maslahi watu wa Jeshi la Polisi, lakini askari hawa wamekuwa wakitumia nafasi zao vibaya kwa masuala binafsi, kwa kuwaonea wananchi. Serikali ina mkakati gani sasa wa kutoa elimu kwa wananchi ili kutambua ofisi hizo za malalamiko ili askari hawa waweze kuchukuliwa hatua kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Geita, vijana wa boda boda na watu wengine wamekuwa wakionewa na Polisi kwa masuala binafsi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Taasisi ya Jeshi la Polisi ina utaratibu wake mahususi wa kuchukua hatua kwa kila askari anapokuwa amefanya makosa na wanafanya hatua hizo hata licha ya kuwa pamekuwepo na mlalamikaji, kwa sababu suala la nidhamu kwenye Jeshi la Polisi ni jambo la kipaumbele hata bila kulalamikiwa, ndiyo maana utaona Askari wetu wana nidhamu kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapotokea matatizo ya aina hiyo, Jeshi la Polisi linachukua hatua. Hata hivyo, niseme tu kwa Waheshimiwa Wabunge na kwa Watanzania kwa ujumla, tunapodai haki ni vyema sana tukatambua kwamba tuna wajibu wa kutimiza na hivyo itaondoa taratibu za kuwepo malalamiko ya mara kwa mara. Kwa sababu katika maeneo mengine unaweza ukamnyooshea kidole askari, lakini ukifuatilia undani wake unakuja kutambua kwamba pana mtu ambaye hakutimiza wajibu wake vizuri ndiyo maana Askari akachukua hatua. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru sana kwa kuniona, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Askari wetu wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana na wanafanaya kazi kwa muda mrefu bila kupanda vyeo mpaka kustaafu. Je, Serikali haioni haja sasa ya kutathmini upya vigezo vya kuwapandisha vyeo ili kuongeza ufanisi wa kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana kwa kutumia weledi wake kama mtumishi wa umma na kutambua umuhimu wa motisha inayoambatana na upandaji wa vyeo kwa askari kama ilivyo kwa Mtumishi mwingine ili kuweza kuongeza ufanisi. Wazo lake ni zuri, tumelipokea na Mheshimiwa Rais alishaongelea kuhusu kuongeza motisha kwa watumishi wa umma wote hapa nchini mara baada ya kuwa ameshamaliza marekebisho na kutoa dira ya Serikali yake. Sisi wasaidizi wake tunatembea kwenye miguu yake, tunatembea kwenye maneno yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwahidi Mheshimiwa Mussa Sima taratibu hizo zitakapoanza kufanyika tutatoa kipaumbele kwa vijana wetu wazalendo wanaolitumikia Taifa kwa uzalendo na kwa moyo wao kwa ajili ya kuhakikisha raia wa Tanzania na mali zao wako salama.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 103

**Uuzaji wa Vifaa hatarishi Barabarani**

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza:-

Kumekuwa na uuzaji holela wa vifaa hatarishi barabarani kama vile visu, mapanga na kadhalika.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukomesha biashara hii ambayo ni hatari kwa usalama wa wananchi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na uuzaji holela wa vifaa hatarishi barabarani. Vifaa hivi hutumika kwa shughuli mbalimbali kama vile kilimo. Hata hivyo vinaweza kutumika vibaya na kuhatarisha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri kwa Halmashauri zetu zote na mamlaka zinazohusiana na biashara kutenga maeneo maalum na kusimamia vema biashara hizo. Aidha, kama hali hii itaendelea Serikali haitasita kuchukua hatua stahiki kukomesha biashara ambayo inaweza ikaleta hatarishi pindi itakapotumika vibaya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella Alex, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, katika jibu lake la msingi amesema kwamba, pindi biashara hii itakapoendelea, Serikali itachukua hatua zinazostahili. Sasa biashara hii ipo inaendelea na hasa katika Majiji makubwa kama Dar es Salaam na ni hatarishi kwa sababu mtu anakuja anajifanya kama anakuuzia kisu, mimi mwenyewe ni muathirika, pindi akikuona umeshika kitu anajifanya kama anakuuzia kisu lakini anakuamuru utoe kile kitu ulichokishika. Sasa naomba tamko la Serikali kwa habari ya biashara hii. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuliona hilo. Kama ilivyo kwa uhalifu mwingine, Serikali inapiga vita uhalifu wa aina yoyote na nitoe rai kwa mtu yeyote ambaye atakutana na mambo ya aina hiyo na yeyote aliye karibu na mtu anayepatwa na jambo hilo, tushirikiane kuhakikisha kwamba tunakomesha uhalifu wa aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi litakuwa bega kwa bega na litakuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba wale wote wanaotumia vibaya mazingira hayo watafikishwa katika mkono wa sheria ili kuweza kukomesha uhalifu wa aina hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa askari hawa ambao wanatekeleza kufanya nchi hii iwe na amani kuhakikisha wahalifu wanakuwa hawafanyi vizuri wako katika Jimbo langu la Itigi na wanakaa katika nyumba ya *railway* ambayo ni mbovu sana.

Kituo kile kiko katika nyumba za *railway;* Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaboreshea Kituo cha Polisi na Mheshimiwa Waziri anajua kabisa kituo kile ni kibovu na hakifai na wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi wamejitahidi kwa nguvu zao wameshindwa. Nini kauli ya Serikali na je, itawasaidia wananchi wa Halmashauri ya Itigi?

**NAIBU SPIKA:** Umeuliza maswali mawili Mheshimiwa Massare. Mheshimiwa Waziri, jibu swali moja tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, natambua mazingira ya kituo kilichopo Itigi na Mheshimiwa Mbunge amekuja mara kadhaa kulielezea jambo hilo na ameandika na barua ya kiofisi na nimemwahidi kwamba kwa hatua ambazo wameshazifanya wao, akiongoza yeye mwenyewe jitihada hizo na sisi kama Wizara tutawaunga mkono na binafsi nitafika katika Jimbo lake kuweza kuongeza nguvu kwa kuona mazingira yaliyopo na hatua ambazo zimeshachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge, nimhakikishie, awahakikishie na vijana wetu kwamba jambo hilo ameshalifikisha na sisi tutalichukulia hatua zinazostahili kwa kulipa uzito unaostahili.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, sasa aulize swali lake.

Na. 104

**Watumishi wa Uhamiaji Ambao Hawajapandishwa Vyeo**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Baadhi ya watumishi wa *DEPU* mwaka 1999 – 2000 na Idara ya Uhamiaji hawajapandishwa vyeo mpaka sasa, licha ya kuwa na vigezo kama vya elimu na ngazi ya shahada huku wenzao wakiwa wamefikia vyeo vya Makamishna na Kamishna wasaidizi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia watumishi kupata haki yao ya vyeo stahiki kama ilivyo kwa wenzao waliopandishwa vyeo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa Idara ya Uhamiaji walioajiriwa mwaka 1999 – 2000 walikuwa na viwango tofauti vya elimu kama vile wengine wakiwemo kidato cha nne, wengine wa kidato cha sita, stashahada na wengine wakiwa na shahada. Katika watumishi wote hao hakuna aliyekuwa amefikia cheo cha Kamishna au Kamishana Msaidizi kama Mheshimiwa Mbunge alivyouliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi hao kwa sasa wametofautiana vyeo kutokana na sababu zifuatazo:-

Moja, waliajiriwa katika vyeo tofauti kulingana na elimu zao wakati wanaajiriwa na kujiunga katika mafunzo ya awali ya uhamiaji.

La pili; baadhi yao walijiendeleza kielimu wakati wapo katika ajira ili kuinua viwango vyao vya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchukuliwa hatua za kinidhamu na kisheria na kupelekea wengine kusimamishwa kupata vyeo kama ambavyo iko kwenye Sheria za Utumishi wa Taasisi hii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, ni wangapi ambao walipandishwa vyeo ambao waliweza kujiendeleza kielimu toka mwaka 1999 na 2000 mpaka sasa na ni utaratibu upi ambao unatumika kupandisha vyeo kwa vijana wa uhamiaji? Kwa sababu mpaka sasa kuna vijana ambao wana vigezo na viwango vya elimu sawa na waliopandishwa vyeo miaka sita nyuma. Kutoka miaka sita mpaka sasa hivi hakuna hata kijana mmoja kwa upande wa Zanzibar ambaye amepandishwa cheo. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatupa sababu ambazo zimepelekea miaka sita mpaka sasa hivi kuwe hakuna mtu ambaye ameweza kupandishwa cheo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, si kwamba hakuna ambaye amepandishwa cheo. Wamepandishwa vyeo katika nafasi tofauti tofauti, kumbukumbu zinaonesha zaidi ya vijana 137 kwa *gap* lile alilolisemea la mwaka 1999 – 2000 walipandishwa vyeo katika nafasi tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wale ambao amesema wa upande wa Zanzibar na lenyewe nitalifuatilia kwa undani wake ili niweze kuwasiliana na Mheshimiwa Mbunge. Kama alichosema ndicho, basi katika hatua zinazofuata

tunakokwenda tutazingatia ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ili kuhakikisha kwamba jambo linapoletwa na watetezi wa wananchi, Waheshimiwa Wabunge, wawakilishi wa wananchi; sisi Serikali tunalifanyia kazi kuhakikisha kwamba panakuwepo na haki ya watu wetu hao wanaofanya kazi vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Askari Magereza wapo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kwa kuwa Askari Magereza na wenyewe wanajiendeleza, wanapata shahada, wanapata elimu ya juu zaidi, lakini mishahara yao imekuwa ikibaki kuwa ile ile ambayo haitofautiani na askari wa kawaida aliye na cheti cha *form four*. Ukiangalia Jeshi la Polisi mtu mwenye shahada anapata sh. 860,000 lakini pia anapata posho ya ujuzi asilimia 15, kwa Askari Magereza wanalipwa sh. 400,000 wakikatwa inabaki 335,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua sasa ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuwalipa Askari Magereza kulingana na ujuzi wao maana imekuwa ikiwaahidi kwamba itawaongezea mshahara kulingana na ujuzi wao, lakini mpaka leo bado. Ni lini sasa itakwenda kuwalipa Askari Magereza kulingana na ujuzi wao ili kuwapa motisha kama askari wengine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko hususan katika masuala mazima ya kupanga mishahara ya Askari Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua katika kada mbalimbali si wote ambao wanapata mishahara ambayo inaendana na kazi zao. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Esther Matiko, tayari tumeshaanza zoezi la tathmini ya kazi na hata ninavyoongea hapa watu wangu wa Bodi ya Mishahara wako hapa Bunge, wameshaongea na Tume ya Huduma za Bunge, lakini vilevile wameshazunguka nchi nzima kuongea na kada mbalimbali. Ifikapo mwezi wa Pili zoezi hili litakuwa limekamilika na baada ya hapo tukae sasa kupanga uwiano wa kazi pamoja na uzito wa majukumu kwa kada moja baada ya nyingine tukitambua ugumu wao wa kazi pamoja na majukumu yao. Vile vile tutaweza kupanga pia miundo yao pamoja na madaraja yao katika ngazi za mshahara. Kwa hiyo, nimhakikishie zoezi hili litaweza kufanyika kwa Askari Magereza, lakini vilevile kwa watumishi wote wa umma kwa ujumla wake.

**NAIBU SIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika!

**NAIBU SPIKA:** Samahani, ngoja nirekebishe jina, Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na matatizo ya askari ambayo yameelezwa, lakini kuna matatizo yaliyoko kwa Askari wetu wa Kikosi cha Reli ambao huwa wanasindikiza hizi treni katika maeneo mbalimbali kama vile Mpanda, Kigoma na Mwanza. Sasa kuna utaratibu wa wao kulipwa *allowance* katika hizo kazi wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Askari wa Kikosi cha upande wa Kata ya Katumba na Ugala wana madai yao tangu mwaka 2013 mpaka sasa hawajalipwa. Sasa je, Waziri yuko tayari kuhakikisha kwamba Shirika la Reli linalipa mafao yao ili waondokane na tatizo la usumbufu kwa sababu imepelekea mpaka wamefungua kesi Mahakamani?

**NAIBU SPIKA:** Ameshaelewa Mheshimiwa. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli yapo malalamiko ya madai mbalimbali ya askari yakiwemo hayo ya askari wale wanaofanya kazi upande wa *TAZARA*. Kilichokuwa kinafanyika ilikuwa ni uhakiki wa madai hayo na Wizara yangu tayari imeshawasiliana na Wizara ya Fedha ili punde ambapo uhakiki huo utakuwa umekamilika wa madai mbalimbali yakiwemo ya askari hao aliowataja Mheshimiwa Mbunge, malipo hayo yaweze kufanyika na kuweza kuondoa kero hiyo ambayo imekuwa ikijitokeza kwa askari wetu wanaofanya kazi nzuri.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Mheshimiwa Tauhida Cassian Galloss, Mbunge wa Viti Maalum, sasa ulize swali lake.

Na. 105

**Wanafunzi Waliopelekwa Kusoma Nje**
**kwa Mwaka 2015/2016**

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS** aliuliza:-

(a) Je, katika bajeti ya mwaka 2015/2016, Serikali imepeleka wanafunzi wangapi kusoma nje ya nchi?

(b) Je, kada gani ambazo zilipewa kipaumbele?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Galoss, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa masomo 2015/2016, Serikali ilipeleka jumla ya wanafunzi 159 katika nchi za China 84, Algeria 57, Urusi wanne (4), Misri wawili (2) na Uingereza kupitia Jumuiya ya Madola 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapeleka wanafunzi nje ya nchi kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa ambavyo ni masomo ya sayansi, teknolojia na TEHAMA. Hivyo wanafunzi wanaopelekwa nje ya nchi husoma shahada ya kwanza, uzamili na uzamivu katika fani za nishati na madini; mfano masuala ya gesi na mafuta, mazingira na mabadiliko ya tabia nchi, uhandisi, afya na sayansi shirikishi, usanifu majengo, elimu, uchumi na mawasiliano.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tauhida Cassian Galoss, swali la nyongeza.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa suala la elimu ya juu ni suala la Muungano, je, wanafunzi wangapi katika idadi ya hao aliowataja wametokea Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, je, wanafunzi hawa wanaporudi masomoni hukuta ajira tayari au wanaachwa wanazurura mitaani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kimsingi nafasi hizi za kusoma nje mara nyingi zinapotolewa zinatangazwa kupitia Balozi husika ambazo zimepanga kutoa masomo hayo, lakini wakati mwingine pia kupitia vyuo vyetu vikuu. Wakati wa uombaji suala linalozingatiwa zaidi ni sifa ikizingatiwa kwamba masuala ya elimu ya juu ni masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wakati mwingine inawezekana kabisa Ubalozi ukaamua kama umependa watu wa Zanzibar, basi utaelekeza moja kwa moja kupitia masuala ya kimahusiano kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kimsingi kwa sasa sitaweza kukupa taarifa kamili na ikizingatiwa kwamba linahitaji *data.* Kwa upande wa ajira, hawa wanafunzi wakirudi, kwa sababu wengi wanakuwa wamepelekwa kwa ajili ya jambo mahsusi, kwa mfano, upande wa gesi, kwa hiyo wanapofika yale maeneo ambayo yanawahitaji ndiyo ambayo yanakuwa yametangaza kazi na wakati huo huo wenye sifa wanakuwa wanachukuliwa kupitia taratibu zetu za kiutumishi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silinde, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Suala la idadi ya wanafunzi ambao wametokana na bajeti linaendana na sifa za wanafunzi wanaotakiwa kujiunga na vyuo vikuu. Ningependa kuuliza swali dogo tu, kwamba, sasa hivi Serikali imetoa kauli mbili tofauti, mwezi Julai iliweka vigezo vya wanafunzi kujiunga na Chuo Kikuu vya *GPA* ya 3.5 kwa watu wa *diploma,* si zaidi ya hapo. Hata hivyo, juzi wametoa tena tamko lingine la *GPA* ya 3.0 kwa watu wa *ordinary diploma.* Je, Serikali itueleze hapa, ni kwa nini inawasumbua wanafunzi katika kipindi hiki ambacho wanafunzi wengi walikuwa wameshakata tamaa na hawaku-*apply* katika Vyuo Vikuu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, kama ambavyo siku Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania analihutubia Bunge; alisisitiza kwamba Awamu hii ya Tano, jukumu lake kubwa litakuwa ni kuongeza ubora. Vile vile lazima ikumbukwe kwamba, Serikali kwa kushirikiana na wananchi imefanya kazi kubwa ya kuwezesha wanafunzi wengi kusoma na kiasi kwamba tunao wengi wenye sifa za ufaulu wa juu. Hiyo imejidhihirisha wazi hata katika udahili wa mwaka huu wa Vyuo Vikuu, waombaji ni wengi na waliofaulu ni wengi sana kiasi cha kupandisha zile *points* ili tuweze kuendana na haki katika kuwachukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika suala hilo katika maeneo hayo pia kuna ushindani mkubwa, lakini Wizara kila wakati inaangalia kama hao watu wenye sifa hizo itaonekana kwamba hawapatikani hapo ndipo tunaweza tukafikiria zaidi namna ya kusema tushuke chini, lakini kama wanapatikana basi hamna haja ya kumchukua mtu ambaye ana ufaulu wa chini ukamuacha mtu ambaye ana ufaulu wa kiwango cha juu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 106

## Kuongezeka kwa Bei za Dawa za Mifugo na Kilimo

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Bei za dawa za mifugo na kilimo zinaongezeka siku hadi siku na kufanya mfugaji mdogo ashindwe kupata maendeleo:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kudhibiti hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulijulisha Bunge Tukufu kuwa asilimia 99 ya dawa zote za tiba na kinga kwa mifugo zinazotumika nchini huagizwa kutoka nje. Jukumu la uagizaji na usambazaji wa dawa na chanjo hufanywa na sekta binafsi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa bei za dawa za mifugo katika baadhi ya maeneo zinaongezeka siku hadi siku. Miongoni mwa sababu zinazochangia kupanda kwa bei hizo ni pamoja na:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, uhaba wa Sekta Binafsi katika baadhi ya maeneo kwa ajili ya kusambaza dawa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, baadhi ya wafugaji kutokuwa na taarifa za kutosha kuhusu namna ya kupata pembejezo za mifugo kutoka kwa mawakala halisi au wasambazaji na hivyo kununua pembejeo hizo kupitia kwa watu ambao huuza kwa bei ya juu wenye malengo ya kupata faida kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza upatikanaji wa chanjo na dawa za mifugo na zenye bei nafuu, Wizara yangu kupitia Taasisi ya Chanjo Tanzania, *(Tanzania Vaccine Institute)* iliyoko Kibaha chini ya Wakala wa Maabara ya Vetenari *(veterinary)* Tanzania inazalisha chanjo dhidi ya magonjwa ya mdondo kwa kuku pamoja na chambavu na kimeta kwa ng'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2015/2016 taasisi imezalisha dozi 30,396,100 za mdondo, dozi ya chambavu 136,800 na dozi 304,300 za kimeta. Aidha, Baraza la Vetenari Tanzania limeendelea kuchukua hatua stahiki

za kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika kuanzisha vituo vya kutolea huduma za mifugo nchini hususan katika maeneo ya wafugaji ili kupanua wigo wa upatikanji wa huduma hizi pamoja na dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zingine zinazochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuondoa ushuru wa kuingiza dawa zote za mifugo zinazoingia nchini na kodi ya ongezeko la thamani *VAT.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwapunguzia wakulima makali ya bei za dawa Serikali kila mwaka imekuwa ikitoa ruzuku ya dawa kwa ajili ya mazao ya korosho na pamba. Pia Serikali imekuwa ikitoa ruzuku kwa ajili ya miche bora inayostahimili magonjwa kwa ajili ya mazoa ya kahawa na chai. Pamoja na ruzuku hizo Serikali imekuwa ikitoa bure dawa za kudhibiti panya, viwavijeshi, kweleakwelea na nzige. Vilevile Serikali imekuwa ikigharamia ndege ya kunyunyizia dawa hizo ili kudhibiti visumbufu hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni tano kwa ajili ya kununua dawa za kilimo na shilingi bilioni moja kwa ajili ya kununua dawa za majosho.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali langu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninalo swali la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wengi wa Mkoa wa Dar es salaam na hasa katika maeneo ya Kitunda, Mvuti, Chanika, Mbande, Pugu, Somangila, Kisarawe II, Kibada, Vijibweni, Yombo, Kunduchi, Mabwepande na Kibamba wote wanategemea kupata vipato vyao na hasa akina mama kwa kwa kazi ya kufuga kuku wa nyama na kuku wa mayai, lakini bei ya dawa zimekuwa kubwa sana kiasi kwamba akina mama hawa wanashindwa kuuza bidhaa zao, wanashindwa kuuza kuku wa mayai na kuku wa nyama kwa gharama ambayo ingeweza kuwapa faida.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga maduka au kuweka dawa katika vituo vya mifugo vya Serikali ambavyo viko katika Wilaya zote Tanzania nzima ili wafugaji hawa waweze kupata nafuu ya bei za dawa kuliko vile wanavyolanguliwa na wafanyabiashara mbaimbali ambao wao hawana uchungu sana na wananchi, wao wanatafuta kipato?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali imeonyesha wazi lengo lake kwamba kuna Kituo cha Tiba cha Kibaha kinaweza kuzalisha chanjo mbalimbali; je, Serikali ina mkakati gani wa kukiongezea nguvu kituo hiki ili iweze kuzalisha chanjo kwa wingi, wananchi waweze kupata chanjo hizo kwa bei nafuu na wao waweze kuboresha vipato vyao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kama alivyosema kwamba kuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa dawa za mifugo, vilevile kwamba bei imekuwa ni bei ambayo wakulima wengi, wafugaji wengi hawawezi kustahimili. Mkakati wa Serikali kwa sasa ni kujaribu kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi ili iweze kutoa huduma hizo, huo ndiyo mwelekeo wa sera tuliyonayo ya mwaka 2006.

Hata hivyo, Serikali kwa kutambua kwamba tayari utaratibu huo una changamoto Serikali inafikiria zaidi kuangalia ni namna gani tunaweza tukawezesha na tukahamasisha ujenzi wa viwanda dawa hizo ziweze kuzalishwa nchini ili bei ipungue. Kwa sababu kinachofanya dawa kwa kiasi kikubwa ziwe ghali ni kwa sababu nyingi tunazitoa nje ya nchi, kwa hiyo kuna utaratibu ndiyo maana tunahamasisha sana kuhusu ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ili kuteremsha na kufanya bei ya dawa hizo kuwa nafuu Serikali imeendelea kupitia wigo wa kodi na tozo mbalimbali ambazo ziko kwenye dawa ili hatimaye dawa hizo ziweze kupatikana kwa urahisi zaidi. Serikali inaendelea kutumia Maafisa Ugani kufanya uhamasishaji na kutoa elimu ili wananchi wenyewe waweze kuona umuhimu wa kutumia dawa ili kuweza kunusuru mifugo yao isife.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili kwamba Serikali ina mpango gani wa kuongezea kiwanda kilichopo Kibaha nguvu, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi waweze kujenga viwanda zaidi. Kwa hiyo, tuko tayari kushirikiana na viwanda hivyo kwa sababu kuna viwanda vya *Farmers Center,* vilevile kuna kiwanda cha *Multivet Services* kwa hiyo zote hizi tutaendelea kufanya nao kazi na kutoa msaada ambao watahitaji ikiwa ni pamoja na msaada ambao watauhitaji ikiwa na nafuu za kodi ili waweze kuzalisha zaidi ili wakulima wetu na wafugaji wetu waweze kupata dawa kwa haraka lakini na kwa bei ambayo ni nzuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea muda wetu umekimbia Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa Mbunge wa Biharamulo Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 107

**Ugonjwa wa Mnyauko wa Migomba- Biharamulo**

**MHE. OSCAR R. MUKASA** aliuliza:-

Biharamulo ni moja ya Wilaya za Mkoa wa Kagera zilizoathirika sana na ugonjwa wa mnyauko wa migomba na hivyo ustawi wa zao hilo kuu la chakula upo mashakani.

Je, Serikali inatoa kauli gani isiyo nyepesi na inayolingana na uzito wa suala hili?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ugonjwa wa unyanjano unasababishwa na bakteria aitwaye *Bacterium Xanthomonas Campetris pv. Musacearum.* Serikali inaendelea kufanya juhudi za kuudhibiti na kuzuia ugonjwa huu nchini kwa kutoa elimu sahihi juu ya unyanjano kwa wadau wote, madhara, ueneaji na udhibiti wa ugnjwa huu. Maeneo ambayo yamezingatia maelekezo ya udhibiti yamefanikiwa kupunguza kasi ya kusambaa kwa ugonjwa huu. Hata hivyo katika kipindi cha ukame ugonjwa wa *black sigatoka* umejitokeza Wilayani Biharamulo na kuleta athari kubwa katika zao la migomba. Ugonjwa huu unasababishwa na Fungi. Ugonjwa huu umejitokeza kuanzia mwezi wa Juni mwaka 2016 baada ya kuanza kipindi cha jua. Maeneo yaliyoathirika ni Nyamahanga vijiji vinne, Bisibo vijiji vinne, Ruziba vijiji vinne, Rusahunga vijiji vinne na Biharamulo vijiji vinne.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia kituo chake cha utafiti kimeelekeza wataalam wa kilimo Wilayani Chato kuwashauri wakulima, kuondoa migomba yenye dalili kali za ugonjwa huo na kupanda mbegu aina ya *FHIA* zinazovumilia ugonjwa huu ambazo kwa sasa mbegu hizi zinapatikana kwa wingi Wilayani humo. Wakulima wakizingatia ushauri huo utasaidia kupunguza usambaaji wa ugonjwa huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, magonjwa ya unyanjano na *black sigatoka* yanaweza kutokomea iwapo wakulima watafuata kanuni bora za kilimo. Aidha, watafiti wetu na wa nchi za Kanda za Afrika Mashariki wanaendelea kutafiti aina ya migomba yenye ukinzani dhidi ya ugonjwa huu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oscar Mukasa swali la nyongeza.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwanza ni amani yangu kwamba wataalamu waliopelekwa kutoa ushauri wa kupelekwa Wilayani Chato ila wamepeleka Wilayani Biharamulo.

Pili maelezo kidogo tatizo hili limekuwepo kwa miaka mingi na tumekuwa tunapata majibu mara nyingi kutoka Serikalini ambayo kwa kweli hayajaweza kukidhi kulingana na ukubwa wa tatizo. Tulisikia swali la kisera kuelekea kwa Waziri Mkuu mwezi wa saba likapelekea kiti chako Mheshimiwa Naibu Spika kutoa maelekezo kwamba Serikali ichukue hatua na ilete majibu hapa.

Sasa swali langu kwa sababu hali halisi inaonesha kabisa kwamba tatizo hili ili likabiliwe kuna mambo matatu lazima yafanyike la kwanza utafiti ili kuja tatizo ni nini ambalo tayari...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oscar Mukasa naomba uulize swali tafadhali umeshatoa maelezo mwanzo sasa uliza swali, ukianza kutaja tena sababu tatu swali tutalifikia saa ngapi.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari kufanya kikao maalum na Wabunge wa Mkoa wa Kagera ili tuone namna gani tunaweka mikakati ya kutafuta utashi wa kisiasa wa kukabili tatizo hili, lakini namna ya kutafuta na kuwashirikisha wadau wengine wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi na hata *private sector* ndani ya Tanzania ili tukabiliane na tatizo hili? Kama uko tayari, upo tayari kwa muda wa karibuni, muda wa kati au muda wa mbali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa KIlimo, Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nilipotaja Chato nilisahau Biharamulo, lakini mimi ndiyo sijasoma kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Biharamulo nayo imo.

Kuhusu ombi lake la kufanya mkutano, tayari nimeshawasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi na ameahidi kwamba tukitoka kwenye Bunge hili atafanya mkutano na Wabunge wanaotoka Mkoa wa Mwanza vilevile Mkoa wa Kagera ili kuangalia namna ya kuweza kushughulikia tatizo hili, kwa hiyo kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge tayari tumepokea na tutafanya haraka tuweze kukutana nao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Nishati na Madini. Mheshimiwa Willy Qulwi Qambalo, Mbunge wa Karatu, sasa aulize swali lake.

Na. 108

**Visima vya Maji Kutumia Mashine za Dizeli**

**MHE. WILLY Q. QAMBALO** aliuliza:-

Katika kupunguza tatizo sugu la maji Wilaya ya Karatu baadhi ya vijiji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wamechimba visima virefu 12 katika maeneo ya Basodawish, Endabash, Rhotia Kainani, Endamarariek, Getamock, Karatu Mjini, Gongali na kadhalika, visima hivyo vinaendeshwa kwa kutumia mashine za dizeli jambo ambalo linasababisha gharama kubwa za uendeshaji.

Je, Serikali itawasidia lini wananchi hao kwa kuwaunganisha na nishati ya umeme katika visima hivyo ili kupunguza gharama za uendeshaji?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kabla sijatoa maelezo ya kuhusiana na swali la Mheshimiwa Mbunge niombe kwa ridhaa ya kiti chako Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wabunge nichukue nafasi moja ya kuwapa pole sana wananchi wa Jimbo langu Chato kwa kupata msiba mkubwa ambao umetokea juzi baada mvua kubwa kunyesha kwenye Jimbo la Chato na kusababisha wananchi wawili kupoteza maisha yao na wananchi wengine 17 kujeruhiwa vibaya sana. Kwa heshima ya kiti chako basi kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge tujumuike na wananchi wa Chato katika kuomboleza msiba huo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Willy Qulwi Qambalo, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya kufikisha umeme katika maeneo yote nchini ikiwa ni pamoja na maeneo ya Wilaya ya Karatu. Kipaumbele katika kutekeleza miradi ya umeme ni pamoja na kufikisha umeme katika miundombinu inayotoa huduma za kijamii ikijumuisha visima vya maji, shule, zahanati, makanisa, misikiti na maeneo ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vya Basodawish, Endabash, Endamarariek, Getamock pamoja na maeneo ya Karatu Mjini yamefikishiwa huduma ya umeme kupitia mradi wa *REA* Awamu ya Pili. Hata hivyo huduma ya umeme haijafikishwa katika visima vya maji vilivyopo katika maeneo niliyoyataja. Kazi ya

kupeleka umeme katika visima hivyo itahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 12.6 na ufugaji wa transfoma tano za KVA 100 kila moja. Gharama ya kazi hizi ni shilingi milioni 467.16. Visima vyote katika vijiji vilivyotajwa hapo juu vitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme katika kisima kilichopo Karatu Mjini inahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 1.2 na kufunga transfoma ya ukubwa wa KVA100. Gharama ya kazi hii ni shilingi milioni 33.81 kazi imepangwa kutekelezwa kupitia bajeti ya *TANESCO* ya mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha vijiji vya Gongali, Gyekrum Lambo, Kainam Rhotia na Kambi Faru vitapata umeme kupitia mradi wa *REA* awamu ya Tatu. Kazi za kuvipatia umeme vijiji hivi itahusisha pia upelekaji umeme kwenye visima vya maji vilivyopo katika vijiji hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Willy Qambalo swali la nyongeza.

**MHE. WILLY Q. QAMBALO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo ya nyongeza pamoja na majibu yenye matumaini ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kisima hiki cha Karatu Mjini kimeombewa umeme sasa ni mwaka mmoja na nusu lakini bado haujaunganishwa na nikiangalia fedha zinazoongelewa kukamilisha kazi ile ni shilingi milioni 33, naona hizi ni fedha kidogo sana kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano Serikali ya Hapa Kazi Tu.

Mheshimiwa Waziri kwa nini Serikali isitafute fedha hizi shilingi milioni 33 ili kisima hiki kiweze kukamilika ili wananachi wapate huduma hii muhimu?

Swali la pili, Awamu ya Tatu ya *REA* inasubiriwa kwa hamu sana katika nchi yetu kwa sababu ni awamu ya kuiwasha karibu Tanzania yote. Hivi sasa tuko mwezi wa tatu ndani ya awamu hiyo; je, ni lini utekekezaji au ujenzi wa miundombinu ya umeme katika maeneo yetu utaanza ili wananchi wetu waweze kujiandaa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mji wa Karatu Mjini kweli ulikuwa upelekewe umeme tangu awamu iliyopita lakini Serikali kulingana na kutoa vipaumbele imetoa shilingi bilioni 33.81 kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, nimhakikishie tu kwamba hizo fedha zitatosha

na isipotosha Serikali bado itatafakari namna ya kuongeza pesa kwa ajili ya kukamilisha mradi huo. Kwa sasa nina uhakika hizo fedha zinatosha na mji wa Karatu Mjini utapata umeme wa uhakika na visima vya maji vyote vitapata umeme kwa kutumia mitambo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Qambalo tumekuwa tukishirikiana sana hata kwenye awamu ya Bunge lililopita. Vijiji alivyotaja ambavyo ni vijiji 21 ambavyo havijapata umeme, nimhakikishie Mheshimiwa Qambalo tumekupelekea umeme vijiji 27 bado vijiji 21 na kati ya vijiji 21 ambavyo bado vimebaki navitambua sana na nimeshafika eneo lile. Kijiji chako cha Endamarariek kitapata umeme, Kambi Faru vitapata umeme hata kule Mbuga Nyukundu itapata umeme kule Rhotia Mbulu kwenye kijiji chako Mheshimiwa Mbunge kitapata umeme pamoja na Mikocheni na Changarawe vyote vitapata umeme.

Kwa hiyo namhakikishia Mheshimiwa Mbunge vijiji vyake vyote ambavyo nimevitaja na ambavyo sijavitaja pia vitapata umeme na kwamba *REA* Awamu ya Tatu inaanza kuingia sasa *site* kuanzia mwezi wa Novemba na mwezi wa Disemba. Hivi sasa wakandarasi wameshapatikana wasimamizi wa kazi wameshapatikana, kazi iliyobaki sasa ni kuanza kutekeleza kwenye kipindi cha mwezi Novemba hadi Disemba. Nimhakikishie vijiji vyake vyote 27 hata kijiji chako Mheshimiwa kile Kijiji cha Kilimamoja kitapata umeme na Kilimatembo bado kitapata umeme. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Willy Qambalo pamoja na majibu yote hayo sijayaona makofi au umepiga ni mimi nilikuwa sioni. Tunaendelea Waheshimiwa Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku Mbunge wa Geita, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

Na. 109

**Wachimbaji Wakubwa Kuwarejeshea Wananchi Sehemu ya Maeneo**

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA (K.n.y. MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA)** aliuliza:-

Sheria ya madini inawataka wachimbaji wakubwa kama vile GGM - Geita, kila miaka mitano wamege sehemu ya maeneo na kuyarudisha kwa wananchi.

(a) Je, ni lini Serikali itawarudishia wananchi maeneo ya Sami na Nyamatagata yaliyoombwa na wananchi kupitia vikao vyote hadi Mkoani?

(b) Je, ni lini eneo la *STAMICO* - Nyarugusu litafanywa kuwa la wachimbaji wadogo wadogo kama ambavyo Mheshimiwa Rais Mstaafu Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alivyokwisha tamka mara mbili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa NIshati na Madini majibu

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, lililoulizwa na Mheshimiwa Bukwimba Mbunge wa Geita Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya maeneo ya Sami pamoja na Nyamatagata yamo ndani ya leseni ya uchimbaji mkubwa wa madini ya dhahabu ya kampuni ya *Geita Gold Mine (GGM)* kupitia leseni namba *SML 45/99.* Hata hivyo Serikali inaendelea na mazungumzo na mgodi huo ili kampuni hiyo iweze kuachia baadhi ya maeneo yasiyohitajika kwa ajili ya kuwamilikisha wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la *STAMICO* na Nyarugusu lipo kitongoji za Buziba lina leseni ya utafutaji Na. *PL 6545/2010 i*nayomilikiwa kwa ubia wa asilimia 45 na 55 kati ya *STAMICO* na kampuni ya *TANZAM 2001,* eseni hii itaisha muda wake tarehe 11 Julai 2018. Kwa kuwa eneo la Nyarugusu bado linamilikiwa na *STAMICO* pamoja na mbia wake ambapo Serikali pia ni mmiliki, Serikali inafanya mazungumzo na wamiliki hawa ili eneo hilo liachiwe sasa kwa ajili ya kumilikishwa wachimbaji wadogo wa eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lolesia Bukwimba swali la nyongeza.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza kabisa nianze kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake, hata hivyo napenda kusema kwa mfano wananchi wa Nyarugusu ni kipindi kirefu sana ni ahadi Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete aliahidi wananchi hawa waweze kupewa eneo hili na harakati mbalimbali, viongozi wengi wamekuja katika eneo hilo kuahidi lakini hakuna kilichofanyika kwa hiyo wananchi wote wa Nyarugusu wanahitaji kusikia kwamba ni lini sasa wataweza kupewa eneo hilo la *STAMICO*?

Swali la pili, wananchi wa Geita wanategemea sana shughuli za uchimbaji ndio maana Wanyamatagata pamoja na Sami na maeneo mengine kama vile Mkaseme maeneo ya Magenge wananchi wanahitaji kupewa

maeneo ya uchimbaji, ningependa kujua sasa nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wananchi hao wanapewa maeneo ya uchimbaji? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na ndugu zangu wa Nyarugusu, nadhani unataka tutoe jibu la ukweli kabisa na hili ndiyo litakuwa la ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba hilo eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge analiongelea ni leseni kati ya *STAMICO* na kampuni ambayo kuna Watanzania na Wacanada, kilichotokea ni kwamba kuna mgogoro mkubwa kweli na Mheshimiwa Naibu Waziri nilivyomuagiza aende kule alivyotoa tamko tu, lile tamko likasambazwa dunia nzima.

Kwa hiyo, naomba wananchi wafahamu kwamba eneo hilo halitatolewa mpaka hiyo kesi iishe. Watanzania tuwe makini sana, tumesaini mikataba na makampuni na mkataba mkubwa ni ule *MDA (Mineral Develepment Agreement),* tukicheza na hiyo kesi na Wabunge kama wanataka tuandikishiane na Wabunge kwamba Serikali ikishtakiwa Wabunge husika watabeba gharama za hiyo kesi kwenye mahakama za nje ya Tanzania. Kesi bado ipo, wananchi wavute subira mpaka hiyo kesi ikamilike kuhusu huo mgodi wa Nyarugusu na huo ndiyo ukweli. Kwa hiyo, ahadi zitatolewa, ahadi zisitolewe tena hapa mpaka hiyo kesi iishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wadogo sasa wa Geita na sehemu zingine, ni kwamba tunatoa maeneo kwa wachimbaji wadogo, na hivi juzi nilikuwa naenda kutoa ruzuku ya awamu ya tatu, lakini tumegundua kwamba ruzuku awamu ya pili waliochukua fedha kwa kupitia *TIB* hawakuchukua fedha walipewa vifaa, vile vifaa vingine havipo huko kwenye migodi.

Kwa hiyo, kabla hatujatoa ruzuku ya awamu ya tatu imesimamishwa mpaka tufanye tathmini ya awamu ya pili na awamu ya kwanza, hapo ndipo tutaenda kutoa ruzuku ya awamu ya tatu. Lakini wachimbaji wadogo Serikali ina dhamira kubwa kwelikweli ya kuwaendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tuheshimu sheria, na ninawaomba Wabunge, tuna Sheria ya Madini ya mwaka 2010 inatambua utoaji wa leseni na *MDAs* hizo. Sasa Wabunge wenyewe hatuwezi kushabikia kuvunja sheria ambazo tuliziweka. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri kwa maelezo lakini Waheshimiwa Wabunge wameshaelewa, hawatataka kuingia huko kuanza kuchangia gharama za kesi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Hawa Ghasia Mbunge wa Mtwara Vijijini, sasa aulize Sali lake.

Na. 110

**Ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini**

**MHE. HAWA A. GHASIA** aliuliza:-

Je, Serikali imeweka mikakati gani ili kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini inayojengwa Mikindani Mtwara?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini, Wizara inaendelea kushirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo katika sekta ya afya ili waweze kuchangia gharama za kukamilisha mradi huu. Vilevile Wizara inaendelea kufanya majadiliano na taasisi mbalimbali za Serikali ambazo zinaweza kutoa mkopo wenye masharti nafuu kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi huu.

Hata hivyo, katika Bajeti ya mwaka 2016/2017, Wizara imetenga jumla ya shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuanza kwa awamu nyingine ya ujenzi wa majengo mengine ya kutolea huduma baada ya kukamilika kwa jengo la matibabu ya magonjwa ya nje *(Out Patient Department)* na mapokezi.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *NHIF* wamekuwa wakitafuta viwanja kule Mtwara kwa ajili ya kujenga kituo kwa ajili ya kutolea huduma za kisasa. Kwa nini wasishirikishwe katika ujenzi huu wa Hospitali ya Kanda ya Kusini badala ya kufanya *duplication* ya kujenga huduma ambazo zinafanana?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa nini Serikali isitenge pesa zake yenyewe kwa kiasi cha kutosha ili kuhakikisha kwamba ujenzi huu unakamilika kwa haraka

kwa sababu umeanza tangu mwaka 2009 na sasa hivi tuko 2016, ni karibia mika saba sasa. Je, wako tayari kutenga pesa zake za kutosha katika bajeti ya mwaka 2017/2018 badala ya kuendelea na mazungumzo ambayo yanaonyesha kutokuzaa matunda?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii, pia namshukuru sana Dada yangu, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Jimbo la Mtwara Vijijini kwa maswali yake mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana kwa jitihada anazofanya kufuatilia ukamilishaji wa mradi huu wa hospitali, yeye pamoja na Mheshimiwa Abdallah Chikota wamekuwa wakinisumbua sana kuhusu utekelezaji wa mradi huu.

Kwa msingi huo mimi mwenyewe nilifanya ziara kwenye mradi huu na mpaka sasa nimekwisha kufanya ziara mbili za kazi na katika ziara moja tuliongozana na wenzetu wa *NHIF* ambao ni Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa ambao upo chini ya Wizara yetu na kuwapa ushauri badala ya wao kujenga hiyo *Center of Excellence* ambayo wamekusudia kuijenga kule Kusini wafanye tathmini na watazame namna ya kutumia fedha zile ambazo walizikusudia kwa mradi wao kuwekeza kwenye kukamilisha mradi huu wa Hospitali ya Kanda ya Kusini, hivyo wazo lake na sisi tulikwishaanza kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lile swali la pili kwamba kwa nini Serikali haitengi pesa za kutosha kwenye bajeti yake; ni kwamba tayari mradi huu umekuwa ukitekelezwa kwa kasi kidogo na Serikali na majengo kwa sehemu kubwa ya kuanzia yamekwisha kukamilika yako takribani asilimia 95 kuanza kutumika na mimi katika ziara zangu nimewaelekeza namna ya kuanza utekelezaji wa mradi wenyewe hivyo hivyo ulipofikia kuliko kuusubiria mpaka ukamilike ili walau huduma za mapokezi, huduma za dharura lakini pia huduma za *out patients* (huduma za wagonjwa wa nje) zianze kutolewa kwa kutumia majengo ambayo tayari yanaelekea kukaimilika kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa tumekwisha kuwekeza takribani shilingi 1,782,000,000, na katika Bajeti ya mwaka 2016/2017, Serikali kwenye bajeti yake imetenga shilingi bilioni mbili kwa ajili ya mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuahidi kwamba tutaendelea kuitazama hospitali hii Ili kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018 tuweze kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya awamu ya tatu ya utekelezaji wa mradi huu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kwa Serikali. Sasa nitaleta kwenu wageni waliotufikia asubuhi ya leo Bungeni.

Kundi la kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge na tutaanza na wageni 42 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira ambao ni kundi la wasanii waliokuja Dodoma kwa ajili ya Tamasha la Fiesta wakiongozwa na Mkurugenzi wa Vipindi na Uzalishaji - *Clouds Media Group,* Ndugu Ruge Mutahaba, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia mnataarifiwa kwamba wasanii hawa wameguswa pia na janga la tetemeko la ardhi lililotokea Mkoani Kagera na watachangia shilingi milioni 40 kwa waathirika. Ahsanteni sana vijana wetu na wasanii wetu kwa zoezi mlilokuja kufanya leo, lakini pia kwa mchango wenu kwa ajili ya maafa ambayo yametupata kama Taifa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni 14 wa Mheshimiwa Rashid Chuachua ambao ni Wajumbe wa *TAYO* na viongozi wa vijana Dayosisi ya Masasi kutoka Masasi, Mkoa wa Mtwara, karibuni sana. Tunao pia wageni 21 wa Mheshimiwa Mussa Sima ambao ni Makatibu Kata wa CCM kutoka Mkoa wa Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Stella Ikupa Alex ambaye ni Mheshimiwa Diwani kutoka Kata ya Ulaya, Jimbo la Mikumi, Mkoani Morogoro, huyu ni Mheshimiwa Matokeo Erasto, karibu sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni 35 wa Mheshimiwa Janet Mbene kutoka *Central Bible College,* Kanisa la *TAG* lililopo Mkoani Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Victor Mwambalaswa ambaye ni ndugu Imelda Mwamanga, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Abdallah Mtolea ambao ni Katibu wake na Msaidizi wake kutoka Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam, karibuni sana. Pia wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Musa Ntimizi ambao ni wadogo zake na pia ni wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Mzumbe kilichopo Mkoani Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Lucy Magereli ambao ni wanafamilia yake kutoka Mkoa wa Dar es Salaam, karibuni sana. Pia kuna wageni 33 wa Mheshimiwa Emmanuel Papian John kutoka shule ya msingi Lalakil iliyopo Kiteto, Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Sikudhani Chikambo ambao ni familia yake kutoka Tunduru Mkoa wa Ruvuma, karibuni sana. Wapo pia wageni wawili wa Mheshimiwa Antony Komu ambao ni wapiga kura wake kutoka Moshi Vijijini, karibuni sana. Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Nditiye ambaye ni ndugu yake kutoka Dar es Salaam, Ndugu Fluoresce King'unza, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Hussein Bashe wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Nzega ambaye ni Ndugu Amos Kanuda, karibuni sana. Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Hilaly Aeshi ambaye anaitwa Haidad Sumry na huyu ni Mjumbe wa Baraza Kuu la UVCCM Taifa na Diwani Kata ya Makanyagio - Katavi, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yapo pia matangazo mengine; mojawapo linatoka kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anawatangazia wageni wote wanaotaka kuchangia kuhusu maafa kwamba watakabidhi michango yao kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu mara baada ya kuahirisha Bunge mbele ya Ukumbi wa Bunge. Kwa hiyo, wale wote ambao wana michango watamkabidhi Mheshimiwa Waziri Mkuu mara baada ya kuahirisha Bunge mbele ya Ukumbi wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo mengine mawili yanatoka kwa Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho kutakuwa na treni ya *deluxe* kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam, yaani tarehe 17 Septemba, 2016. Mheshimiwa Waziri anawataarifu Wabunge kwamba kesho kutakuwa na hiyo treni maalum ambayo imetayarishwa kwa ajili yao, yaani kwa ajili yenu ninyi Waheshimiwa Wabunge, na treni hiyo itaondoka saa 2.00 asubuhi kuelekea Dar es Salaam. Kwa hiyo, wale wote ambao wanajitayarisha na safari hii wanaweza kumuona Mheshimiwa Waziri au pia wajue kuwahi saa 2.00 asubuhi treni ya *deluxe* itaondoka kuelekea Dar es Salaam.

Tangazo lingine linalotoka kwa Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa ni tangazo kuhusu ndege mbili za kwanza, zile ambazo zimeagizwa na Serikali na kwamba ndege ya kwanza kati ya hizo mbili itawasili siku ya Jumanne, tarehe 20 Septemba, 2016. Mheshimiwa Waziri anasema ndege hiyo itapokelewa na viongozi Wakuu katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere *(Julius Nyerere International Airport)* Dar es Salaam. Waheshimiwa Wabunge watakaokuwa na nafasi wanakaribishwa kushiriki mapokezi hayo, muda wa kuwasili ndege mtataarifiwa katika vyombo vya habari.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa tarehe 20 Septemba, 2016 uwanja wa ndege. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka Utawala, mnakumbushwa kwamba zoezi la usajili...

Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane kwa sababu mpaka sasa hivi kuna Wabunge hawajajisajili sasa watakapougua baada ya hili tangazo, tusikilizane ili tusije tukaanza kutafutana baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, mnakumbushwa na Utawala wa Bunge kuwa zoezi la usajili kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umeendelea tangu mwezi Februari, 2016 hadi Mkutano huu wa Nne wa Bunge, hivyo basi Wabunge wote ambao bado hawajajisajili na mfuko huu wanakumbushwa kufanya hivyo kwani mwisho wa usajili ni leo, tarehe 16 Septemba, 2016. Mnakumbushwa kuzingatia sana suala hili kwa sababu ni muhimu kwa ajili ya afya zetu.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine pia linatoka Utawala, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa hapo mwanzo mlitaarifiwa kuwa Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) inaandaa mafunzo maalum kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge. Kufuatia wito huo Waheshimiwa Wabunge mtakaopenda kushiriki kwenye mafunzo hayo mnatakiwa kuwasilisha majina yenu kwa Ndugu Suleiman Mvunye ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi Huduma kwa Wabunge, tafadhali muandike simu hii kwa ajili ya mawasiliano ya karibu, 0657 728237. Aidha, tangazo hili haliwahusu Waheshimiwa Wabunge ambao tayari wamekwishajiorodhesha kushiriki mafunzo hayo, kwa hiyo ni wale ambao hawajajiandikisha ili waende pia wakajisajili.

Tangazo lingine tena la Utawala, Waheshimiwa Wabunge mnakumbushwa kuwa wataalam wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* bado wapo hapa Bungeni kwa ajili ya zoezi la ugawaji wa vitambulisho hivyo na usajili wa Wabunge ambao bado hawajajisajili. Hivyo basi, Waheshimiwa Wabunge wote ambao mliweza kujisajili na *NIDA* mnaombwa mfike kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa katika chumba kilichokuwa kinatumika kama zahanati ili mpatiwe vitambulisho vyenu kabla hamjandoka. Aidha, Waheshimiwa Wabunge ambao hamkuwahi kujisajili mnaombwa mfike katika ukumbi huo kwa ajili ya usajili na pia kuchukua vitambulisho vyenu.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo yalikuwa matangazo yetu tunaendelea. Katibu!

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Anatropia Theonest.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 68(7) na kwa sababu ya wakati naomba nisiisome.

Nimepata taarifa kwenye Ofisi yangu juu ya kinachoendelea hasa kupanda kwa gharama ama kupanda kwa ada katika Vyuo Vikuu vya Afya nchini na hasa Chuo cha St. Francis, MUHAS, Hubert Kairuki na vyuo vingine. Kumekuwa na bei elekezi kutoka *TCU (TCU guide)*. Wanafunzi hawa wamekuwa waki-*report* vyuoni na kukuta bei tofauti na bei elekezi kutoka vitabu hivyo vya *prospectus* au *TCU guide*. Imeenda mbali zaidi mfano kama *TCU guide* ya Chuo cha Mwanza inaonesha ada yake ni shilingi milioni 3.7 lakini wanafunzi walivyo-*report* chuoni wamekuta gharama ni shilingi milioni 4.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wa vyuo umeji-*organize* na kupeleka malalamiko yao walichoambulia wanafunzi hawa ni kutishiwa kufukuzwa vyuo. Hali kadhalika chuo cha St. Francis wameenda mbali zaidi, awamebadilisha hata *prospectus* tofauti na bei za awali wameandika kitu kipya na kuleta bei mpya. Naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hii Kanuni pengine bahati mbaya Mheshimiwa Anatropia Theonest akasema hatoisoma kwa kuangalia muda, lakini pengine angepata fursa ama mimi ningemwambia aisome asingefikia kwenye kutoa maelezo aliyoyatoa.

Waheshimiwa Wabunge, inawezekana kweli hilo tatizo lipo kwa sababu mimi sina taarifa nalo, lakini Waheshimiwa Wabunge ukitumia Kanuni ya 68(7) unakuwa unazungumzia mambo yaliyotokea Bungeni mapema. Kwa hiyo, ni lazima jambo litokee kwanza Bungeni, hilo ni la kwanza.

Pili, unataka kumuuliza Spika, je, jambo hilo lililotokea linaruhusiwa au haliruhusiwi? Ndiyo maana ya Mwongozo, kama unataka jambo lingine unatumia kanuni zingine siyo Kanuni ya 68(7). Kwa hiyo, Mheshimiwa Anatropia Theonest mwongozo kwenye jambo hilo haupo, kwa sababu hilo jambo halijatokea Bungeni mapema.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu!

**MHE. RIZIKI S. NGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Riziki samahani naomba ukae, Katibu!

**NDG. NENELWA WANKANGA - KATIBU MEZANI**:

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**NAIBU SPIKA:** Miswada ya Sheria ya Serikali, Katibu!

**NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kuweka Masharti na Kuimarisha Taaluma na Weledi katika Tasnia ya Habari, Kuundwa kwa Bodi ya Ithibati ya Wanahabari, Kuanzishwa kwa Baraza Huru la Habari, Kuweka Mfumo wa Usimamizi wa Huduma za Habari Pamoja na Mambo yanayohusiana na hayo *(A Bill for an Act to provide for legal framework for the promotion of professionalism in the Media Service Industry establish Journalist Accreditation Board, Independend Media Council and Framework for Regulation of Media Services and provide for other related matters)*.

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya marekebisho katika Sheria Mbalimbali zipatazo tisa kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws)*.

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Miswada miwili imesomwa kwa mara ya kwanza yaani Muswada wa Sheria ya Huduma za Habari wa mwaka 2016 *(The Media Services Bill, 2016)* na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2016 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill,* 2016) na Mheshimiwa Spika ataipeleka kwenye Kamati zinazohusika ili ziweze kuifanyia kazi na sisi Waheshimiwa Wabunge tutapata fursa ya kushiriki katika mchakato mzima.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo Mheshimiwa Spika, atakuja kuendelea na ratiba kama inavyoonesha kwenye orodha ya shughuli zetu za leo. *(Makofi)*

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu!

**NDG. NENELWA WANKANGA - KATIBU MEZANI:** Taarifa ya Katibu wa Bunge.

**SPIKA:** Taarifa ya Katibu wa Bunge.

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**DKT. THOMAS D. KASHILLILAH - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 29(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye orodha ya shughuli kwa ajili ya kufanyiwa kazi katika Mkutano wa Nne wa Bunge, zimekamilika.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Katibu wetu kwa taarifa hiyo kwamba shughuli zetu zilizopangwa kwa Mkutano huu wa Nne sasa zimekamilika. Katibu!

**NDG. NENELWA WANKANGA - KATIBU MEZANI:**

**HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**SPIKA:** Naomba kumuita Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutulinda na kutupa afya njema hadi kutufikisha siku ya leo tunapohitimisha Mkutano wa Nne wa Bunge lako Tukufu tulilolianza tarehe 6 Septemba, 2016. Nitumie fursa hii pia kukupa pole kwa maradhi yaliyokusibu lakini kikubwa nieleze furaha yangu kwa uponyaji ambao Mwenyezi Mungu amekujaalia na hivi sasa tupo pamoja humu ndani, tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu uendelee kupata nguvu na afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu tulipokutana mara ya mwisho kumekuwepo majanga na matukio mbalimbali ya maradhi, ajali, ujambazi na matukio mengine ambayo yamesababisha vifo na majeruhi kwa Watanzania wenzetu wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, hivyo ninatoa pole kwa wafiwa wote na wale wote waliopatwa na majanga kutokana na matukio hayo, tunawaombea afya njema wale wote waliopata majeraha na walioko hospitali pia.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunahitimisha Mkutano huu tukiwa tumekamilisha shughuli zote zilizopangwa kwenye Mkutano huu. Naomba nitumie fursa hii ya awali kabisa kukupongeza sana wewe Mheshimiwa Spika,

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kukamilisha kazi zote kwa ufanisi mkubwa. Kazi hizo zilijumuisha kujadili na hatimaye kupitisha Miswada mbalimbali ya Serikali. Napenda kukiri kwamba mijadala ya Mkutano huu ilikuwa ya wazi na hoja zilizotolewa zililenga kuiletea maendeleo nchi yetu. Kutokana na michango mizuri ya Waheshimiwa Wabunge na yenye tija ilibidi mara kadhaa vikao vyetu kuendelea hadi usiku nje ya muda wa Kikanuni, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Kuhusu tukio la janga la tetemeko la ardhi lililotokea katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kuwa tarehe 13 Septemba, 2016 Serikali iliwasilisha hapa Bungeni taarifa ya masikitiko kuhusu maafa makubwa yaliyoikumba nchi yetu tarehe 10 Septemba, 2016 kutokana na tetemeko la ardhi lililotokea katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa ya Kagera, Geita, Mwanza na Mara. Tukio hilo ambalo liliathiri zaidi Mkoa wa Kagera lilitokea siku ya Jumamosi majira ya saa 9.27 alasiri ambako Mji wa Bukoba ulikumbwa na tetemeko la ardhi lenye nguvu ya mtetemo wa kipimo cha 5.7 kwa kutumia *scale* ya *richter*.

Tetemeko hilo limesababisha vifo vya watu wetu 17 na majeruhi 253. Napenda nitumie nafasi hii kwa mara nyingine kuwapa pole wafiwa wote na wale wote waliopata majeraha mbalimbali, tunaomba Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi na kwa wale waliopata majeraha tunamuomba Mungu awaponye haraka.

Mheshimiwa Spika, tukio hilo limesababisha uharibifu mkubwa sana wa nyumba, vituo vya afya, shule pamoja na miundombinu ya barabara. Aidha, shule nne za Nyakato, Ihungo, Kashenge na Buhembe zimeharibika ikiwemo vyoo, nyumba za walimu, kumbi za shule, mabweni na nyumba 840 zimeteketea kabisa, nyumba 1,264 kupata nyufa. Kwa sasa uongozi wa Mkoa wa Kagera pamoja na Kamati ya Maafa ya Mkoa na wataalam kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, wataalam wa masuala ya matetemeko na wadau wengine wanaendelea kufanya tathmini ya kina ya kiasi cha hasara iliyopatikana.

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako Tukufu lilivyojulishwa, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imechukua hatua kadhaa kushughulikia athari za tetemeko hilo ikiwa ni pamoja na kufanya jitihada ya kurejesha hali ya utulivu na miundombinu iliyoharibika ili kuirejesha katika hali ya kawaida. Pamoja na jitihada mbalimbali zilizofanyika ikiwemo viongozi kutembelea maeneo yenye madhara, mpaka sasa Serikali imefanya mambo yafuatayo:-

Kuhusu chakula, wananchi wenye mahitaji ya chakula wameendelea kupatiwa chakula kama vile unga, mchele, maharage, sukari, chumvi pamoja na mafuta kula. Tathmini ya kubaini mahitaji halisi ya chakula inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matibabu, Serikali imeimarisha Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera kwa kupeleka dawa na vifaa tiba kupitia Bohari Kuu ya Dawa. Aidha, timu ya wataalam na madaktari 12 wamepelekwa Bukoba kutoka Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando. Ninapenda kuwashukuru pia wadau mbalimbali ambao wamechangia eneo hili wakiwemo *Medecins Sans Frontiers,* Ubalozi wa China, *Jhpiego (USAID)* na Chama cha Wafamasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu makazi; wananchi waliokosa kabisa hifadhi ya makazi wamepewa maturubai na mahema kwa ajili ya makazi ya muda. Aidha, waathirika ambao nyumba zao zimebomoka kabisa kwa kuanzia kila mmoja ametengewa mabati 20, saruji mifuko mitano, *blanket* na mikeka pia wapangaji waliokuwa katika nyumba hizo kila mmoja ametengewa kodi ya pango ya miezi sita ili apate mahali pa kujihifadhi kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu shule zilizoathirika Serikali inajenga miundombinu ya muda ya shule kama vile madarasa, mabweni na vyoo hususani katika shule za sekondari za Ihungo na Nyakato zilizofungwa kwa muda wa wiki mbili. Tathmini ya kitaalam ikikamilika mpango wa ujenzi wa miundombinu ya kudumu itafanyika na maandalizi yanaendelea kupata rasilimali kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazishi; Serikali imeshiriki katika kuwafariji wafiwa lakini pia kushiriki mazishi kwa kusaidia kutoa jeneza, sanda, usafiri na kutenga fedha shilingi milioni 20 za rambirambi kwa ajili ya wafiwa ambazo zitatolewa kwao muda wowote kuanzia sasa. *(Makofi)*

Kuhusu barabara; tathmini ya uharibifu wa barabara imefanyika na barabara zilizoharibika zitarejeshwa katika hali ya kawaida ili wananchi waendelee kupata huduma za msingi. Vilevile Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuharakisha miundombinu ya majisafi na majitaka inakarabatiwa na kuhakikisha usafi unaendelea kuwa katika viwango stahiki. Kwa ujumla Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa taasisi za umma zikiwemo majeshi ya ulinzi na usalama na rasilimali zake vinatumika kutoa huduma zote muhimu kwa waathirika katika kipindi hiki cha matukio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali inaendelea kufanya tathmini ya kitaalam kupitia Wizara ya Nishati na Madini, Chuo cha Madini Dodoma na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kubaini chanzo cha tukio, kiasi cha athari zilizotokea chini ya miamba na juu ya ardhi. Tathmini hii ya kitaalam itatupa picha ya mwelekeo wa kushughulikia urejeshaji wa miundombinu iliyoharibika.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii pia kukushukuru sana wewe binafsi, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge kwa namna mlivyoshirikiana na Serikali katika kushughulikia janga hili la Kitaifa la tetemeko la ardhi. Napenda

kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu ya hali na mali na kwa kututia moyo katika kushughulikia tukio hili kubwa lilioathiri sana maisha na shughuli za wananchi pale Mkoani Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa niaba ya Serikali na kipekee nitumie fursa hii kuishukuru Jumuiya ya Wafanyabiashara nchini, Waheshimiwa Mabalozi, Wawakilishi wa Mashirika ya Umma na ya Kimataifa waliopo nchini, viongozi wa Vyama vya Siasa na wananchi kwa ujumla ambao waliitikia wito wa Serikali kwa kushiriki na kusaidia juhudi za Serikali za kuwasaidia waathirika wa tetemeko la ardhi. Tunawashukuru sana wote waliotuunga mkono kwa fedha na vifaa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo zinazofanywa, Serikali imeshatoa na inaendelea kukusanya michango kutoka kwa wananchi na wadau mbalimbali. Hivyo, kwa wananchi na wadau walio tayari kuchangia wanaweza kutumia akaunti ya maafa iliyofunguliwa katika Benki ya *CRDB* yenye Namba 0152225617300 kwa jina la Akaunti - Kamati Maafa Kagera yenye *swift code CORUtztz* kwa kutuma fedha kwa njia ya kawaida au hata pia *mobile banking*. Vilevile michango hiyo inaweza kutumwa kwenye namba za simu za mkononi zifuatazo:-

*M-PESA* 0768 196 669 au namba ya *Airtel Money* 0682 950009 au namba ya *Tigo Pesa* 0718 069 616. Nawaomba wananchi wote, sekta binafsi na Jumuiya za Kimataifa tuoneshe mshikamano kuungana na Serikali katika kusaidia wenzetu walioathirika na tetemeko hilo kwa kutoa michango ya hali na mali.

Mheshimiwa Spika, nitumie pia fursa hii kuwahakikishia Watanzania wote kuwa Serikali itaendelea kuratibu michango yote kwa uaminifu mkubwa itakayotolewa na kufikishwa kwa walengwa kama ambavyo imekusudiwa. Aidha, Serikali itaendelea kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa kuimarisha uwezo wetu wa ndani wa kukabiliana na majanga ya aina hii na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, shughuli za Bunge; tunahitimisha Mkutano huu tukiwa tumepata fursa ya kujadili Miswada, Maazimio na Kauli mbalimbali za Mawaziri. Miswada iliyowasilishwa na Serikali na kusomwa kwa Mara Pili na pia kusomwa kwa Mara ya Tatu na ni kama ifuatavyo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Habari wa mwaka 2016 *(The Access to Information Bill, 2016);*

(ii) Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa mwaka 2016 *(The Valuation and Valuers Registration Bill, 2016);*

(iii) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa mwaka 2016 *(The Government Chemist Laboratory Authority Bill, 2016);*

(iv)Muswada wa Sheria ya Usimamizi na Wanataaluma wa Kemia wa mwaka 2016 *(The Chemist Professionals Bill, 2016);*

(v) Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo wa mwaka 2016 *(The Tanzania Agricultural Research Institute Bill, 2016);* na

(vi) Muswada wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi wa mwaka 2016 *(The Tanzania Fisheries Research Institute Bill, 2016).*

Mheshimiwa Spika, Miswada ya Sheria ya Serikali iliyosomwa kwa mara ya Kwanza ni pamoja na Muswada wa Sheria wa Huduma ya Habari ya mwaka 2016 *(The Media Services Bill, 2016)* na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa mwaka 2016 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment (No. 3) Bill, 2016).*

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili Serikali ilitoa kauli zifuatazo:-

(i) Kauli ya Serikali kuhusu hali ya chakula nchini na uzalishaji kwa msimu wa mazao kwa mwaka 2015/2016 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2016/2017.

(ii) Kauli ya Serikali kuhusu tukio la tetemeko la ardhi lililotokea tarehe 10 Septemba, 2016, Mkoani Kagera na Mikoa mingine ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wataalam wake kwa mchango wao mkubwa katika kuandaa Miswada hiyo, kwa umakini mkubwa na hivyo kuwawezesha Waheshimiwa Mawaziri kuiwasilisha Bungeni kwa weledi mkubwa.

Aidha, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri, Serikali itazingatia ushauri wenu na maoni yenu tote yaliyotolewa kwa utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu pia jumla ya maswali 110 ya msingi na mengine 222 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Vilevile, jumla ya maswali matano ya msingi na ya nyongeza ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu ya kila Alhamisi yaliulizwa na kupata majibu.

Mheshimiwa Spika, mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi. Katika siku za hivi karibuni kumekuwepo na wasiwasi kuhusu mwenendo wa hali ya uchumi hususan mtiririko wa fedha kwenye uchumi wa Taifa.

Napenda kutumia fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kuwa mwenendo wa uchumi ni wa kuridhisha na unaendelea kuimarika. Aidha, tathmini iliyofanyika kuhusu viashiria vya uimara wa sekta ya fedha inaonesha kuwa mabenki yetu bado yapo salama na yana mitaji ya kutosha na mwenendo wa sekta ya fedha ni wa kuridhisha.

Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango, Benki Kuu ya Tanzania na Taasisi ya Taifa ya Takwimu zinafuatilia kwa karibu sana kuhusu mwenendo wa hali ya uchumi nchini. Mathalani, tarehe 14 Septemba, 2016, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Profesa Benno Ndulu, alitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu mwenendo wa hali ya uchumi nchini ambapo alilihakikishia Taifa na Jumuiya ya Kimataifa kwamba hali ya uchumi wetu ni shwari kabisa na si mbaya kama inavyodhaniwa na baadhi ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika taarifa hiyo ya Benki Kuu, pamoja na mambo mengine, imebainisha kwamba katika robo ya kwanza ya mwaka 2016, ukuaji wa uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa wa kuridhisha. Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 5.5 ikilinganishwa na asilimia 5.7 kipindi kama hicho mwaka 2015. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme, huduma za mawasiliano, utangazaji na huduma za *internet,* kuongezeka kwa uchimbaji na madini. Pia shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi ya juu katika kipindi hicho ni sekta ya fedha kwa asilimia 13.5, mawasiliano asilimia 13.4 na utawala wa umma asilimia 10.2.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mwenendo huo mzuri wa viashiria vya shughuli za uchumi, ni dhahiri kwamba mwelekeo wa uchumi katika kipindi kijacho unatoa matumaini ya uchumi kuendelea kuimarika kama ilivyokadiriwa hapo awali na kufikiwa kwa lengo la ukuaji wa Pato la Taifa la asilimia 7.2 kwa mwaka 2016. Hii inachangiwa pia na ukweli kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga vizuri katika kuimarisha uchumi endelevu, usimamizi thabiti wa rasilimali za umma na ujenzi wa miundombinu bora yenye kuimarisha lengo la kujenga uchumi wa viwanda chini ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa mwezi Julai na Agosti, 2016. Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuchukua hatua mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, mapato ya Serikali yanatarajiwa kuongezeka na hivyo kupunguza utegemezi wa kibajeti kutoka

kwa washirika wa maendeleo. Aidha, Serikali inaendelea kudhibiti utoaji wa misamaha ya kodi ili kuleta tija kwa Taifa katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imelenga kukusanya mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri ya jumla ya shilingi trilioni 18.46, sawa na asilimia 62.5 ya bajeti yote ya shilingi trilioni 29.5. Takwimu za mwenendo wa ukusanyaji mapato zinaonesha kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Agosti, 2016 mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* yalikuwa shilingi trilioni 2.168 ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya shilingi trilioni 2.11, sawa na asilimia 103 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, aina ya kodi zinazochangia sana katika ongezeko hilo ni pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya mashine za kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato. Mapato yasiyo ya kodi kwa kipindi hicho yalikuwa shilingi bilioni 271.1 sawa na asilimia 60 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 448.4. Aidha, mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri yalikuwa shilingi bilioni 45.4, ikiwa ni asilimia 41 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 110.9. Napenda kutumia fursa hii kuzihimiza Wizara na Halmashauri kuongeza jitihada za ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuendelea kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo ya biashara, viwandani, migodini, bandarini, kwenye viwanja vya ndege na maeneo ya mipakani ili kuhakikisha kuwa kodi stahiki zinakusanywa;

(ii) Kusimamia kikamilifu matumizi ya vifaa vya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato;

(iii) Kuendelea kupanua wigo wa walipa kodi ikiwa ni pamoja na kurasimisha sekta isiyo rasmi ili iweze kuingia katika mfumo wa kodi;

(iv)Kuimarisha ufuatiliaji wa mapato yanayokusanywa na taasisi na mamlaka mbalimbali za Serikali na Halmashauri zote nchini; na

(v) Kuendelea kuchukua hatua za kudhibiti na kupunguza misamaha ya kodi isiyokuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali wa kuhamia Dodoma. Tarehe 23 Julai, 2016 Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akihutubia Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi hapa Dodoma alieleza kuhusu dhamira ya Serikali ya Awamu ya

Tano ya kukamilisha mchakato wa ahadi ya Serikali ya kuhamia katika Mji wa Makao Makuu wa Dodoma.

Aidha, Mheshimiwa Rais alirejea kauli hiyo tarehe 25 Julai, 2016 wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Mashujaa nchini ambayo ilifanyika Kitaifa kwa mara ya kwanza katika Viwanja vya Mashujaa, Mjini Dodoma. Mheshimiwa Rais alisisitiza kuwa anatarajia kwamba Serikali yake yote itakuwa imehamia Dodoma katika kipindi cha miaka minne na miezi minane iliyobaki hadi kufikia mwisho wa mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba mpango wa sasa wa Serikali wa kuhamia Dodoma ni mwendelezo wa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 iliyozingatia agizo lililotolewa tarehe 1 Oktoba, 1973 kwenye Mkutano Mkuu wa 16 wa Chama cha *TANU.* Hivyo, hatua zinazochukuliwa sasa na Serikali ya Awamu ya Tano ni mwendelezo tu wa utekelezaji wa mipango ya awali iliyokuwa inatekelezwa mwaka hadi mwaka na Serikali za awamu zote zilizopita, kuanzia Awamu ya Kwanza lilipotolewa tamko hilo mwaka 1973 chini ya uongozi wa Rais wa Awamu ya Kwanza na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hiyo ya Serikali ya Awamu ya Tano, baada ya tamko la Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli la tarehe 23 Julai 2016, yafuatayo yamefanyika:-

(i) Tarehe 26 Julai nilikutana na viongozi wa Mkoa wa Dodoma (viongozi wa chama na Serikali wa Mkoa na Wilaya, Wazee Maarufu, Viongozi wa Madhehebu ya Dini na wadau mbalimbali) ili kuwajulisha kuhusu mkakati wa sasa wa Serikali wa kuhamia Dodoma. Aidha, niliutaka uongozi wa Mkoa wa Dodoma kuwasilisha mapendekezo ya mpango kazi wa kutekeleza uamuzi wa Serikali wa kuhamia Dodoma kwa Wanadodoma wenyewe.

(ii) Katika kipindi cha siku 14, uongozi wa Mkoa wa Dodoma uliwasilisha kwangu Taarifa ya Serikali kuhamia Dodoma kama ilivyokusudiwa. Aidha, tarehe 15 Agosti, 2016, Mkoa uliwasilisha mpango huo katika Kikao cha Baraza la Kazi la Mawaziri pamoja na Makatibu Wakuu na kupata ushauri na maoni yao ya kuuboresha.

(iii) Serikali imeunda Kamati Ndogo chini ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma *(CDA)* kwa lengo la kufanya mapitio ya upatikanaji wa ofisi, makazi na miundombinu muhimu. Kamati hiyo itashirikisha taasisi mbalimbali za Serikali zilizopo Dodoma na Kitaifa zikiwemo *TBA, DUWASA, TANROADS, TEMESA, TANESCO, SUMATRA, TTCL,* Jeshi la Polisi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

(iv) Aidha, Serikali imeunda Kamati ya Kitaifa ya Makatibu Wakuu ambao wanaratibu zoezi zima na utaratibu wa Serikali kuhamia Dodoma.

(v) Tarehe 1 Septemba, 2016, Serikali ilikutana na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Fedha, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Sekta Binafsi zinazohusika na ujenzi wa miundombinu nchini. Lengo la kikao hicho lilikuwa ni kupata mawazo ya sekta binafsi, taasisi za fedha na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuisaidia Serikali kuboresha mkakati wa kuhamia Dodoma kwa kuzingatia kuwa Serikali peke yake haiwezi kukamilisha jambo hili.

Katika kikao hiki tumekubaliana kwamba kuanzia sasa kuwepo na vikao baina ya Makatibu Wakuu na wadau wa sekta binafsi angalau mara moja kwa mwezi chini ya Uenyekiti wa Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Kamati hiyo akiwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu. Kikao hicho kitakuwa cha mashauriano na kupeana mrejesho wa utekelezaji wa azma ya Serikali ya kuhamia Dodoma kwa kuzingatia mchango wa sekta ya umma na sekta binafsi katika ujenzi wa miundombinu ya kiuchumi na kijamii, uwekezaji, uzalishaji, biashara na huduma mbalimbali.

(vi) Serikali pia imeunda Kamati Maalum ya Wataalam Washauri itakayoshirikiana na *CDA* katika kufanya mapitio ya mpango kamambe *(master plan)* wa Mji wa Dodoma ili kubaini mahitaji halisi ya sasa na siku zijazo katika upeo wa miaka 50 na zaidi. Zoezi hili linahitaji ushirikishwaji mkubwa wa jamii na sekta binafsi. Lengo la Serikali ni kuwa na mji uliopangwa vizuri na unaozingatia vigezo mbalimbali vya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ya Awamu ya Tano inatambua jitihada kubwa zilizofanywa na Serikali za Awamu zilizopita zilizoongozwa na Chama cha Mapinduzi na kuweka miundombinu mbalimbali muhimu ya kufanikisha mpango wa Serikali kuhamia Dodoma. Tathmini iliyofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma pamoja na wadau mbalimbali, inaonesha kuwa kwa ujumla miundombinu iliyopo Dodoma kwa sasa ina uwezo wa kutosheleza mahitaji ya Serikali kuhamia Dodoma kwa awamu kuanzia mwezi huu wa Septemba, 2016 hadi 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ratiba ya Serikali kuhamia Dodoma; ili kufanikisha azma ya Serikali kuhamia Dodoma, tayari imeandaliwa ratiba itakayowezesha Serikali kuhamia Dodoma kwa awamu kuanzia Septemba, 2016 hadi 2020 bila ya kuathiri bajeti yetu ya mwaka 2016/2017 kama ifuatavyo:-

(i) Awamu ya kwanza itakuwa kati ya Septemba, 2016 na Februari, 2017. Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote, Makatibu Wakuu wote, Manaibu Makatibu Wakuu wote watahamia Dodoma katika awamu ya kwanza. Aidha,

kila Wizara itatakiwa kuwahamisha watumishi wa idara moja au mbili na wakati huo huo kuendelea kuweka utaratibu wa kuleta watumishi wa idara nyingine kuhamia Dodoma. *(Makofi)*

(ii) Awamu ya pili itakuwa kati ya Machi, 2017 na Agosti, 2017. Kipindi hiki kitawapa fursa watendaji wa Wizara mbalimbali kuweka katika bajeti zao za mwaka 2017/2018 gharama za kuendelea kuhamisha watumishi wake kuja Dodoma. *(Makofi)*

(iii) Awamu ya tatu itakuwa kati ya Septemba, 2017 na Februari, 2018 ambapo Wizara zitaendelea na uhamishaji wa watumishi wa idara zilizo ndani ya Wizara zao.

(iv) Awamu ya nne itakuwa kati ya Machi, 2018 na Agosti, 2018.

(v) Awamu ya Tano itakuwa kati ya Septemba 2018 hadi Februari, 2020.

Katika kipindi hiki cha awamu ya tatu na nne, Wizara zitakuwa zinaendelea pia kuhamisha watumishi wake.

(vi) Awamu ya sita itakuwa kati ya Machi, 2020 na Juni, 2020 ambapo Ofisi ya Rais ikiongozwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, watakuwa wanafika Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazishauri Wizara zote katika zoezi hili la kuhamia Dodoma, kuanzisha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu wa kielektroniki badala ya kuhama na mafaili kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma na tunataka Dodoma iwe ya kielektroniki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuwakaribisha wawekezaji mbalimbali wa sekta binafsi na wadau wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi kuwekeza Dodoma ili kuboresha zaidi miundombinu iliyopo na kuongeza majengo ya ofisi na makazi ya watumishi, kuwekeza katika huduma za afya, elimu, huduma za biashara kama mabenki, maduka makubwa *(shopping malls)* na masoko, mahoteli na maghala. Aidha, napenda kurejea maelekezo niliyoyatoa kwa Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma *(CDA)* na Mkoa wa Dodoma na Manispaa kuhakikisha kwamba Mji Mkuu wa Dodoma unaendelezwa kwa kasi ili kupokea watumishi wengi na familia zao pamoja na sekta binafsi watakaohamia Dodoma.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa Mkoa wa Dodoma na *CDA* wahakikishe kuwa pamoja na kuandaa maeneo ya makazi na ofisi, pia watenge maeneo maalumu ya huduma muhimu kama vile maeneo kwa ajili ya

kituo kikuu cha biashara, bustani, bandari kavu na kuendelea kuongeza eneo la viwanda na huduma mbalimbali za kibiashara. Aidha, naagiza Mamlaka za Mipango Miji Mkoani Dodoma na hasa *CDA* wahakikishe wanaweka mfumo wa kielektroniki wa upatikanaji wa viwanja ambao utatambua mahitaji kwa utaratibu wa wazi na bila urasimu usio wa lazima. Vilevile nashauri wakazi wa Mkoa wa Dodoma na sekta binafsi kutumia fursa hii sasa kujenga nyumba za kuishi za kutosha, nyumba za kulala wageni na mahoteli ili watumishi na wageni watakaokuja Dodoma wasipate taabu kutafuta mahali pazuri pa kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya kilimo; hali ya uzalishaji na upatikanaji chakula nchini. Tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2015/2016 iliyofanyika mwezi Juni, 2016 ilionesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula Kitaifa utafikia tani 16.1. Aidha, mikoa 11 kati ya 26 ilibainika kuwa na ziada ya chakula, mikoa 12 kuwa na utoshelevu wa chakula na miwili uhaba wa chakula. Kutokana na mahitaji ya chakula kwa mwaka 2016/2017 kuwa tani milioni 13.1, nchi itakuwa na utoshelevu wa chakula kwa asilimia 123 sawa na ziada ya tani milioni tatu kwa mazao yote ya chakula.

Mheshimiwa Spika, tathmini hii ilibaini pia kuwa chakula kingi aina ya nafaka kilikuwa tayari kimesafirishwa nje ya nchi kutokana na nchi jirani kutokuwa na mavuno mazuri bila kuzingatia haja ya utoshelevu wa ndani ya nchi kwanza. Ili kuhakikisha kuwepo kwa hali ya usalama wa chakula nchini na kuepuka baa la njaa hapo baadaye, Serikali imeamua kuanzia tarehe 10 Septemba, 2016, sehemu ya ziada ya nafaka ya mahindi na mchele itasafirishwa nje ya nchi kwa vibali vitakavyotolewa kwa utaratibu wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi pekee. Serikali itasimamia ili kusiwe na upungufu wa chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwataka Wakuu wa Mikoa yote nchini kuwahamasisha wakulima na wafanyabiashara kuongeza thamani ya mazao ya kilimo hususan mahindi na mpunga kwa kuyasindika kabla ya kuyasafirisha nje ya nchi ili yapate bei nzuri zaidi na pia kuzalisha ajira kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo katika msimu wa kilimo 2016/2017; kuanzia mwaka 2003/2004 hadi 2015/2016, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya chakula na hususan mahindi, mpunga na mtama. Pia ruzuku ya pembejeo hutolewa kwa mazao ya biashara ya korosho, pamba, chai, kahawa na alizeti. Ruzuku hiyo imekuwa ikitolewa kwa kutumia mfumo wa *voucher* na vikundi vya wakulima kukopeshwa pembejeo hizo kupitia taasisi za fedha na makampuni ya pembejeo ya kilimo. Pamoja na juhudi hizo, kumekuwepo na changamoto mbalimbali katika kufikia lengo hilo.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi, katika msimu wa 2016/2017, Serikali imetenga shilingi bilioni tano kwa ajili ya ruzuku ya viuatilifu vya mazao ya kilimo na shilingi bilioni 25 kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo nyingine za kilimo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 20 ni za kununua tani 21,892 za mbolea kwa kaya 354,928. Aidha, Serikali italipia asilimia 30 ya bei ya mbolea kwenye soko sawa na shilingi 20,000 kwa mfuko wa kilo 50 wa mbolea ya kupandia na shilingi 12,000 kwa mfuko wa kilo 50 wa mbolea ya kukuzia.

Mheshimiwa Spika, ili mbolea hizo ziweze kuwafikia walengwa kwa wakati na kwa bei nafuu, Kampuni ya Mbolea Tanzania itasambaza mbolea katika vituo vyake 29 nchini na kuiuza kwa mawakala wa pembejeo za kilimo kwa shilingi 38,000 kwa mfuko wa kilo 50 kwa mbolea ya kupandia na shilingi 26,000 kwa mfuko wa kilo 50 wa mbolea ya kukuzia. Ninaziagiza Halmashauri zote kuhakikisha mawakala wa pembejeo wanauza mbolea kwa bei itakayopangwa. Ni imani yangu kuwa wakulima wengi watatumia fursa hii ya kupata mbolea ya ruzuku kuendeleza kilimo cha kisasa, chenye tija na cha kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya ushirika. Maboresho katika tasnia ya ushirika. Kwa muda mrefu sasa ushirika kama chombo cha kuwaunganisha, kuwapa nguvu na kuwatetea wanachama wao katika kilimo, ufugaji, uvuvi na tasnia nyingine, unakabiliwa na changamoto nyingi za usimamizi mbovu, ubadhirifu na ufujaji wa mali wa baadhi ya viongozi. Changamoto hizo zinawaumiza sana wakulima na kuwafanya kukata tamaa katika uzalishaji, masoko na uendeshaji wa shughuli zao za uchumi. Ili kuondokana na changamoto hizo, Serikali itafanya marekebisho makubwa ndani ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika iliyo chini ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na kuchukua hatua za kinidhamu kwa watakaobainika kuhusika na ubadhirifu wa mali za ushirika. Aidha, baadhi ya Maafisa Ushirika waliokaa katika kituo kimoja kwa muda mrefu watahamishiwa katika maeneo mengine. Serikali itafanya marekebisho makubwa vilevile kwa Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika *(COASCO)* ambalo limeshindwa kufanya kazi zake kwa weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kufufua ushirika, Serikali itahuisha Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya 2002 na kuijengea Tume ya Maendeleo ya Ushirika uwezo wa kuajiri/kuhamishia watendaji katika ofisi za Mikoa na Halmashauri zote ili kusimamia vyama vya ushirika; kufanya kaguzi za mara kwa mara; kuondoa tatizo la upotevu wa rasilimali za vyama; kusimamia upatikanaji wa viongozi wenye sifa na watendaji wenye weledi wenye kuongoza vyama kwa ufanisi; kupanua wigo wa shughuli za ushirika katika sekta nyingine za kiuchumi zaidi ya kilimo ili kuongeza idadi ya vyama vya ushirika nchini na hivyo kuchochea ukuaji wa kipato cha wananchi walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya elimu. Motisha kwa Walimu Wakuu na Waratibu Elimu Kata. Katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na usimamizi mzuri na wa karibu shuleni, Serikali imeanza kutoa posho ya madaraka kwa Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Waratibu Elimu Kata kila mwezi kuanzia Julai, 2016 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 5.09 tayari kimeshatolewa. Aidha, mpango mwingine uliopo ni kuwapatia Waratibu Elimu Kata pikipiki ili ziwawezeshe katika ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli za kielimu katika kata zao nchi nzima. Kwa kuanzia, Waratibu Elimu Kata wa Mikoa saba ambayo ilikuwa na ufaulu wa chini katika matokeo ya kuhitimu darasa la saba tayari wameshapatiwa jumla ya pikipiki 1,015. Mikoa iliyopatiwa pikipiki hizi pamoja na idadi ni kama ifuatavyo:-

(i) Mkoa wa Dodoma pikipiki 192;
(ii) Mkoa wa Mara pikipiki 99;
(iii) Mkoa wa Simiyu pikipiki 122;
(iv) Mkoa wa Shinyanga pikipiki 128;
(v) Mkoa wa Tabora pikipiki 200;
(vi) Mkoa wa Kigoma pikipiki 135; na
(vii) Mkoa wa Lindi pikipiki 139.

Mheshimiwa Spika, Mikoa iliyobakia itapatiwa pikipiki chini ya Programu ya Kukuza Stadi za Kusoma na Kuandika ya *LANES (Literacy and Numeracy Education Support Program)* pamoja na *UNICEF*.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa walimu na miundombinu; kwa upande wa upungufu wa walimu, Serikali imeamua walimu wapya watakaoajiriwa mwaka 2016 wapangwe shuleni moja kwa moja na kwenye maeneo yenye upungufu mkubwa wa walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya madawati; utakumbuka kuwa tarehe 16 Machi, 2016, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli alitoa agizo kwa Wakuu wa Mikoa kuhakikisha kuwa ifikapo tarehe 30 Juni, 2016 kusiwepo mwanafunzi anayekaa chini kwa kukosa dawati. Katika utekelezaji wa agizo hili la Mheshimiwa Rais, kufikia mwezi huu wa Septemba madawati 951,610 kwa shule za msingi yalitengenezwa na hivyo kufikia madawati 3,084,781 sawa na asilimia 94.4. Kwa upande wa shule za sekondari, idadi ya madawati yaliyotengenezwa yamefikia madawati 1,490,488 sawa na asilimia 99.4 na kufanya upungufu wa madawati kuwa madawati 182,864 kwa shule za msingi na 8,380 kwa shule za sekondari. Madawati hayo yanaendelea kutengenezwa na Mikoa ambayo haijakamilisha inatakiwa iwe imeshakamilisha zoezi hilo ifikapo tarehe 30 Septemba, 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu maabara katika shule za sekondari; mahitaji ya maabara kwa shule za sekondari ni 10,803. Maabara zilizopo ni 5,756 sawa na asilimia 53.2 ya mahitaji. Upungufu uliopo wa maabara ni 5,047 ambazo zingine

zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri imetenga jumla ya shilingi bilioni 18.8 kwa ajili ya umaliziaji wa maabara 2,135 katika shule za sekondari kwenye Halmashauri mbalimbali nchini. Serikali inaendelea na ujenzi wa jumla ya maabara 290 kupitia mpango wa MMES II katika shule za sekondari 528. Upungufu utakaokuwepo baada ya kukamilika kwa maabara hizi ni maabara 4,807. Serikali itaendelea kubuni mikakati mbalimbali ya kuondoa upungufu huo.

Mheshimiwa Spika, suala la mitihani ya elimu ya msingi; mtihani wa kumaliza darasa la saba ulifanyika tarehe 7 na 8 Septemba, 2016 nchini kote. Idadi ya watahiniwa walikuwa ni 795,761 waliosajiliwa kufanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2016. Aidha, taarifa za awali zinaonesha kuwa takriban watahiniwa 789,302 walifanya mtihani huo sawa na asilimia 99.2 ya waliosajiliwa. Taarifa rasmi itatolewa baada ya Mikoa na Halmashauri kukamilisha kufanya mawasilisho ya taarifa kamili kupitia Baraza la Mitihani na baada ya mitihani hiyo kufanyika.

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya idadi ya kubwa ya wanafunzi waliofanya mitihani ya darasa la saba ni kwamba yapo matarajio makubwa kuwa idadi ya wanafunzi watakaoingia kidato cha kwanza mwaka 2017 itakuwa kubwa vilevile kuliko nafasi zitakazokuwepo mwanzoni mwa mwaka 2017 katika shule za sekondari ikiwa hali ya miundombinu itaendelea kuwa kama ilivyo sasa. Hivyo basi, natoa wito kwa Halmashauri zote nchini zijiandae kuwawezesha wanafunzi wote watakaofaulu kujiunga na kidato cha kwanza kwa kuongeza vyumba vya madarasa, madawati, matundu ya vyoo na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Spika, uhakiki wa vyeti kwa watumishi. Serikali imeendelea na zoezi la uhakiki wa vyeti vya watumishi ingawa limeendelea kuleta usumbufu kwa watumishi katika baadhi ya maeneo. Naagiza kwa Wakurugenzi kuandaa vituo maalum kwa zoezi hilo vilivyo jirani na vituo vya wafanyakazi huko mahali pa kazi badala ya kuwakusanya eneo moja jambo ambalo linaleta usumbufu ili kuwapunguzia pia adha na gharama. Halmashauri zote zizingatie agizo hili ili kwamba Maafisa Utumishi waende kwenye maeneo ya watumishi hao kwa kupanga vituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii pia kuzungumzia kidogo kuhusu jitihada za Serikali za kuimarisha usafiri wa anga hapa nchini kuanzia mwaka 2016/2017. Serikali ya Awamu ya Tano inaendelea na mpango wake wa kuboresha usafiri wa anga hapa nchini. Hatua zinazochukuliwa sasa ni pamoja na kuendelea kuboresha viwanja vya ndege nchini. Lengo ni kuhakikisha kuwa kila Mkoa angalau unakuwa na kiwanja cha ndege cha kisasa chenye ubora unaofaa kutua ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kwenda sambamba na azma ya Serikali kuhamia Dodoma muda mfupi ujao, kiwanja cha ndege cha Dodoma kimefanyiwa ukarabati mkubwa ili kuweza kuhudumia ndege zenye uwezo wa kubeba abiria mpaka 90. Sambamba na hatua hizo, Serikali imedhamiria kuimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)* ikiwa ni pamoja na ununuzi wa ndege mpya kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa huduma za usafiri wa anga kupitia *ATCL. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imenunua ndege mbili aina ya *Dash 8-Q400* zenye uwezo wa kubeba abiria 76 kila moja zitakazotumika kutoa huduma za usafiri wa anga kwa soko la ndani na nchi jirani.  Ndege hizo zinatarajia kuwasili nchini mwezi huu wa Septemba, 2016. Aidha, taratibu za kununua ndege nyingine mbili zenye ukubwa wa kati *(medium haulage aircraft)* zitakazokuwa na uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 110 zimeanza. Ndege hizo zitahudumia soko la kikanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hiyo Serikali imeanza kazi ya kuiunda upya *ATCL,* imeshaanza na jana tarehe 15 Septemba, 2016, Mheshimiwa Rais amefanya uteuzi wa Mtendaji Mkuu mpya wa *ATCL.* Aidha, mchakato wa uteuzi wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika hilo unakamilishwa. Vilevile Serikali imegharamia mafunzo ya wataalam mbalimbali wakiwemo wahandisi watakaohudumia ndege mpya. Hatua hizo zitasaidia sana kuboresha Shirika letu la Ndege na usafiri wa aga hapa nchini katika kipindi kifupi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vimeendelea kulinda na kudumisha amani na utulivu uliopo nchini kwa manufaa ya ustawi wa nchi yetu. Usalama wa raia na mali zao umeendelea kudumishwa kwa kutambua kuwa ni miongoni mwa misingi mikuu ya ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Kwa namna ya pekee, napenda kutumia fursa hii kuvipongeza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kufanya kazi hiyo kwa weledi.

Mheshimiwa Spika, ili Jeshi la Polisi liendelee kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kubaini, kuzuia na kukabiliana na uhalifu nchini, Serikali itaendelea kuwajengea uwezo maafisa wetu, wakaguzi na askari wote na pia kutekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kutabiri mwelekeo wa uhalifu kwa kutumia takwimu za uhalifu, kumbukumbu za uhalifu pamoja na mabadiliko ya uhalifu ili kuweza kutambua maeneo korofi, wahalifu watakaohusika, mahali walipo na namna ya kukabiliana nao na uhalifu huo.

(ii) Kuyatambua maeneo nyeti *(hot spots)* yenye vivutio vya uhalifu na kuyapangia ulinzi, misako na doria imara.

(iii) Kutoa elimu kwa jamii kuhusu mbinu mbalimbali za kuzuia na kupambana na uhalifu kwa kutumia vyombo vya habari, mihadhara, mikutano, maonesho na usambazaji wa machapisho na vipeperushi.

(iv) Kufanya misako na doria mara kwa mara ili kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo mbalimbali nchini.

(v) Kushirikiana na wadau wote wa ulinzi na usalama, kubadilishana taarifa za kiintelijensia pamoja na uzoefu katika kuzuia uhalifu kwa kuibua mifumo mipya na kuboresha ya zamani.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa suala la amani na usalama na utulivu nchini halina mbadala. Nawaomba tudumishe hali ya amani na usalama ili tufanikishe lengo letu la kukuza uchumi na kuondoa umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, nchi yetu imeendelea kuwika kimichezo kupitia mchezo wa soka. Nitumie nafasi hii kuipongeza sana timu yetu ya Taifa ya Vijana chini ya umri wa miaka 17 kwa ushindi mkubwa wa mechi zilizotangulia dhidi ya Seychelles kwa kupata mabao tisa kwa sifuri, dhidi ya Afrika Kusini mabao matatu kwa moja na kwa sasa timu yetu inajiandaa kupambana na nchi ya Congo tarehe 18 Septemba, 2016 kuelekea fainali za Afrika. Natoa wito kwa Watanzania tuungane pamoja kuiombea timu yetu, kuipa *support* timu yetu ili iweze kufanya vizuri kwenye mashindano yake yajayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho, wakati tunahitimisha mkutano huu leo, napenda nitumie nafasi hii kukushukuru sana wewe binafsi Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia Naibu Spika, niwashukuru pia Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Bunge kwa kusimamia vizuri na kwa weledi mkubwa vikao vyote vya Mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa michango yenu. Ninashukuru pia watendaji wa Serikali kwa kuwasaidia Mawaziri na Manaibu Mawaziri katika kujibu maswali na hoja mbalimbali za Wabunge. Niwashukuru pia madereva wote kwa kuwaendesha Mawaziri, Wabunge na watendaji wote kwa usalama kabisa. Niwashukuru pia wanahabari kwa kusaidia kurusha na kuihabarisha jamii juu ya kinachoendelea Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na timu yake kwa kutuwezesha kukamilisha shughuli zetu zote za Mkutano huu kwa mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tunahitimisha Mkutano huu leo na kuelekea katika Majimbo yetu, sote tunatambua kuwa msimu wa mvua za vuli na masika unakaribia. Hivyo, napenda kutumia fursa hii kuziagiza Wizara zinazohusika na usambazaji wa pembejeo kuhakikisha zinawafikia wakulima kwa wakati na kwa bei iliyopangwa. Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wawahakikishe kwamba wanasimamia kikamilifu shughuli za kilimo katika maeneo yao ili kila familia na kaya ianze maandalizi ya kilimo mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kurejea katika kusisitiza kuwa sekta binafsi ndiyo injini ya kukuza uchumi katika Taifa letu. Hivyo, nichukue fursa hii kuwahakikishia wafanyabiashara na wenye viwanda na wawekezaji kwa ujumla kuwa Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kuwapa ushirikiano wa dhati ili kuendeleza shughuli zao kama ambavyo wamepanga. Wafanye shughuli zao bila woga au bila matishio yoyote yale.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini si kwa umuhimu, nitumie muda huu kumwomba Mwenyezi Mungu awalinde na awaongoze Waheshimiwa Wabunge wote katika safari ya kurejea majumbani kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi tarehe 1 Novemba, 2016, siku ya Jumanne, saa 3.00 asubuhi litakapokutana katika Ukumbi huu hapa Dodoma, Makao Makuu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa Waheshimiwa Wabunge na imeungwa mkono. *(Makofi)*

Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yako nzuri sana. Baada ya hotuba hiyo nzuri sasa naomba niwahoji kuhusu hoja ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameitoa na hoja yenyewe inahusiana na suala la kuahirisha Bunge mpaka tarehe ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameitaja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliridhia kuahirishwa Bunge mpaka Tarehe 1 Novemba, 2016, Saa Tatu Asubuhi, Mjini Dodoma)*

**SPIKA:** Wengine wanataka kulowea humu? *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba niseme maneno machache hapa tunapomalizia shughuli zetu, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwamba Bunge litaanza tarehe 1 Novemba, 2016, saa 3.00 asubuhi. Kamati za Bunge zitaanza vikao vyake tarehe 17 - 30 Oktoba, 2016 hapa hapa Dodoma. Wakati wenzetu Serikali wanaendelea kujipanga kuhamia Dodoma sisi tumeshahamia *full-fledged.* Shughuli zetu zote ni hapa Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, muendelee kujipanga na kwa ambao mtahitaji viwanja Dodoma nijue mapema iwezekanavyo, nawahakikishieni wote mnaweza kupata viwanja. Pia watumishi wa Serikali ambao wanategemea kuhamia Dodoma kutoka Dar es Salaam na mahali pengine wanaohitaji viwanja tunawahakikishia wote wanaweza kupata viwanja. Dodoma ni pana, Dodoma ina uhakika, inapangika, tuna muda wa kutosha wa kutengeneza Mji Mkuu tunaoutaka sisi Watanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa wale wasiofahamu lakini angalau *UDOM* mnaijua, kwa wale waliotembelea *UDOM* ina kama hekta 5,000 kwa ukubwa wake na upana wake na mnaona zile taasisi zilivyotawanyika. Sasa Makao Makuu ya Serikali peke yake patakapojengwa ofisi za Serikali kule Ihumwa na maeneo mengine zimetengwa hekta 20,000, ni mara nne ya *UDOM*, kila Wizara itakuwa na eneo kubwa, la kutosha na kubaki. Kwa hiyo, Dodoma inatosha kabisa kwa sisi wote na tutaenea kabisa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru wote kwa jinsi ambavyo tumeendesha Mkutano wetu huu wa Nne vizuri, kwa salama na amani. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye pia ndiyo Kiongozi wa Wabunge walio wengi kwenye lugha ya bibi kule wanaita *majority leader,* lakini pia nimpongeze Kiongozi wa Upinzani Bungeni kwenye Mabunge ya wenzetu wanamuita *minority leader* kwa kuyaongoza makundi yao mawili vizuri na kufika mahali ambapo tumeweza kufanya kazi vizuri bila migogoro yoyote katika Mkutano huu Nne. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Watanzania wanapenda hali hii, Watanzania hawapendi kuona vurugu kubwa, msambaratiko maana msambaratiko ukianzia hapa unaenda na kwa wananchi wetu, umoja ukiwa hapa unaenda na kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa jinsi mlivyoendesha mambo yenu katika kipindi hiki kwa salama na amani, tuendelee na utaratibu huu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mahudhurio kwenye kazi za Kamati ukiondoa Kamati ya *PAC*, Kamati nyingi zilizobaki mahudhurio yake si mazuri sana. Si mazuri kwa baadhi ya Mawaziri na si mazuri kwa baadhi ya Wabunge. Naomba huko tunakoenda tuzingatie sana mahudhurio kwa pande zote mbili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumetengeneza orodha ya watoro, Mawaziri watoro, Wabunge watoro kwenye kazi za Kamati lakini nimesema niitunze niangalie na kikao kijacho. Kama watoro wale wataendelea basi tutawaambia waajiri wao kwa maana ya wapiga kura wenu na kwa maana ya vyama vyenu kwamba Mbunge huyu na Mbunge huyu na Mbunge huyu kwa chama chenu kazi za Bunge hafanyi ili hivyo vyama vijue. Kwa upande wa Mawaziri basi tutamwambia namba moja kwamba hawa hawawajibiki. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, ningependa mahudhurio kwenye shughuli za Bunge yawe mazuri kwa sababu tunazitaja mapema kama hivi tumesema Kamati zitaanza tarehe 17 – 30 Oktoba, 2016, hii inatoa nafasi ya ku-*adjust* ratiba zetu angalau kwa yale ambayo yanayopangika yaweze kupangika. Kama alivyosema Waziri Mkuu tarehe 1 Novemba, 2016 tunaanza vikao vya Bunge, kwa hiyo, inatoa nafasi kwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge kupanga ratiba zenu vizuri na mapema. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI na Madawa ya Kulevya wamekuwa wakilalamika sana kwamba hawana kazi za kutosha za kufanya. Tumeendelea kutafakari jambo hili na tutaendelea kulifanyia kazi, mpaka Kamati zitakapoanza tarehe 17 Oktoba, 2016 tutakuwa tumeshafanya maamuzi ya msingi. Tutaona njia ya kufanya endapo masuala haya ya UKIMWI na Madawa ya Kulevya tuyarudishe kwenye Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii au vinginevyo, lakini kwa hakika kwa sasa hivi tutawatawanya Wajumbe wote wa Kamati ya UKIMWI kwenda kwenye Kamati nyingine. Tutawasiliana tutakapokuwa tumeyaweka vizuri mambo haya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba Tanzania ilikuwa Mwenyeji na Mwenyekiti wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alikuwa ndiye Mwenyekiti hivi majuzi. Miongoni mwa mambo yaliyozungumzwa kwenye kikao hicho kilichofanyika Ikulu - Dar es Salaam tarehe 8 Septemba, 2016 ilikuwa ni suala la Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kusaini Makubalianao ya Mafungamano ya Kiuchumi *(Economic Partnership Agreements -EPA)* na Jumuiya ya Ulaya. Kilichokubaliwa katika mkutano huo ni kuahirisha kutia saini makubaliano hayo mpaka Januari, 2017 ili Kamati ya Wataalam ifanyie kazi maeneo yenye kuhitaji kupitiwa upya kwa maslahi mapana ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hakika hatuna budi kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu katika suala hili kwa kuweka mbele maslahi ya Tanzania na Afrika Mashariki, lakini pia kwa diplomasia ya hali ya juu aliyoweza kuionyesha kiasi cha makubaliano hayo kufikiwa kwamba hali halisi itazamwe kwa Afrika Mashariki kwa pamoja. Hivyo basi, ni matumaini ya Bunge hili sasa

kwamba kupitia kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali italisimamia kikamilifu suala hili na kwa wakati muafaka litaletwa hapa Bungeni ikiwezekana kwenye Mkutano wa Bunge ujao ili tuweze kujadili na kuishauri Serikali ipasavyo. Naamini Mheshimiwa Waziri Mkuu mtalichukulia suala hili kwa uzito unaostahili ili Wabunge waweze kulijadili na kuweza kuishauri Serikali vizuri endapo tusonge mbele na jambo hilo kama nchi au vinginevyo kabla Serikali haijafanya maamuzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo kutoka kwa Mheshimiwa William Ngeleja, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* kwamba Jumapili ya tarehe 25 Septemba, 2016, Wabunge wapenzi wanachama wa Simba na wale wa Yanga watakuwa na mechi kwenye Uwanja wa Taifa Jijini Dar es Salaam. Fedha zitakazopatikana kutokana na mechi hiyo zitapelekwa kusaidia waathirika wa tetemeko la ardhi Mkoani Kagera. Mechi hiyo itatanguliwa na mpambano kati ya timu za *Bongo Flavor* na *Bongo Movie* na kutakuwa na burudani kutoka kwa wasanii mbalimbali. Ratiba ya mazoezi ya timu ya *Bunge Sports Club* itatumwa kwa wachezaji kupitia mtandao.

Narudia tena Waheshimiwa Wabunge, tarehe 25 Septemba, 2016 kutakuwa na mechi muhimu sana pale Uwanja wa Taifa, tunawaomba wananchi hasa wa kule Dar es Salaam wajitahidi kujitokeza na Waheshimiwa Wabunge mtakaokuwepo kule siku hiyo ni vizuri kufika tuweze kuangalia yale yote yaliyoandaliwa kwa ajili yetu siku hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, palisomwa hapa kwa Mara ya Kwanza Miswada ya Sheria ya Serikali, napenda kuwaambia kwamba nakala za Miswada hiyo tayari yote iko kwenye *pigeon holes* zenu. Kwa hiyo, kila atakayetoka hapa apitie pale ili wakati shughuli za Kamati zinapoanza usije ukasema huna nakala.

Narudia tena, nakala za Miswada iliyosomwa Mara ya Kwanza leo iko kwenye *pigeon holes* zenu, mnapotoka hapo nje kila mmoja apitie. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho kwa upande wangu ni kwamba kila Mheshimiwa Mbunge unapotoka hapa upite pale Jengo la Utawala *(ground floor),* kuhusu masuala fulani fulani ya utaratibu sasa ikitokea Mbunge umeondoka bila kupita pale usije ukamlaumu Spika.

Narudia tena, kila Mbunge ukitoka hapa pita pale *ground floor* ni muhimu sana, kuna mambo yanayohusu utaratibu, mambo ya walimu na nini kuyaweka sawasawa. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni Wimbo wa Taifa, naomba wote tusimame.

*(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa)*

**SPIKA:** Baada ya Wimbo huo wa Taifa, naomba sasa nichukue fursa hii kuahirisha shughuli za Bunge hadi tarehe 1 Novemba, 2016, siku ya Jumanne, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 6.07 mchana Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumanne,*
*Tarehe 1 Novemba, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*